Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

Toleo la 08

# Jarida la HEET UDSM

**Toleo la Julai - Oktoba 2025**

HEET
Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi




**Ushirikishwaji wa Wadau** *Waonesha Mafanikio katika Mradi wa HEET UDSM* — Ukurasa 25


## Ndani ya toleo hili...


Ukurasa 8 — **Mapitio ya Mtaala** *Yafikia Hatua ya Mwisho*

Ukurasa 11 — **UDSM Yaongoza Mradi wa HEET Ukikamilika kwa** *74% Kitaifa.*

Ukurasa 23 — **Ujumbe kutoka Sudani Kusini** *Wapongeza Maendeleo ya Mradi wa HEET UDSM*









# YALIYOMO


| | |
|---|---|
| 3 | Salamu za Makamu Mkuu wa Chuo |
| 4 | Ujumbe wa Mratibu |
| 5 | Ujenzi wa Mradi wa HEET Wachochea Matumaini na Fursa Mpya Buyu - Zanzibar |
| 6 | Mpango wa Kujenga Uwezo Wakuza Viwango vya Kitaaluma na Utendaji UDSM |
| 8 | Mapitio ya Mtaala Yafikia Hatua ya Mwisho, Programu Mpya 32 zapata Ithibati |
| 9 | Programu ya Uambatishaji Wafanyakazi wa UDSM Kwenye Tasnia Yabadilisha Mtazamo wa Kitaaluma |
| 10 | Mfumo wa Ushughulikiaji Malalamiko Wafanikisha Uzingatiaji Madhubuti wa Taratibu katika Utekelezaji wa Mradi wa HEET |
| 11 | UDSM Yaongoza Mradi wa HEET Ukikamilika kwa 74% Kitaifa |
| 13 | Vifaa vya Kisasa Vyabadili Elimu ya Wenye Mahitaji Maalum UDSM |
| 14 | Viongozi Wasisitizwa Kuwa Kichocheo cha Utafiti na Ubunifu |
| 15 | Ujumbe wa Naibu Mratibu |
| 16 | Tahariri |
| 18 | Matukio katika Picha |
| 20 | Mikakati ya KASEMA Yaimarisha Uendelevu wa Mradi wa HEET na Ushirikishwaji wa Jamii |
| 22 | Uzingativu wa Hatua za Usalama na Ushirikishwaji wa Jamii Vyaimarisha Utekelezaji wa Mradi wa HEET |
| 23 | Ujumbe kutoka Sudani Kusini Wapongeza Maendeleo ya Mradi wa HEET UDSM |
| 25 | Ushirikishwaji wa Wadau Waonesha Mafanikio katika Mradi wa HEET UDSM |
| 27 | HEET Yaizatiti UDSM Kufundisha Programu 98 kwa Njia ya Mtandao na Njia Mseto |

# Salamu za Makamu Mkuu wa Chuo



**Prof. William A. L. Anangisye**

**Makamu Mkuu wa Chuo**

Kwa niaba ya Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ninawakaribisha wasomaji wetu katika Toleo la Nane la Jarida la HEET-UDSM. Kama ilivyo ada, tunawafahamisha wadau wetu kuhusu maendeleo ya Mradi.

Kupitia jarida hili, wadau wetu siyo tu wanapewa taarifa kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa Mradi wa HEET, bali pia wanapata wasaa wa kutoa maoni yao kuhusu Mradi huo.

Chuo chetu kimeendelea na ufuatiliaji na tathmini ili kuhakikisha kuwa kunakuwa na mafanikio ya malengo ya maendeleo ya Mradi. Katika jarida hili, wasomaji wanapewa fursa ya kujifunza kuhusu maendeleo yaliyopatikana tangu toleo lililopita.

Tunafurahi kuwajuza hatua iliyofikiwa ya mapitio ya mitaala kwamba, mitaala 32 imekwishaidhinishwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania. Wakati shughuli za ujenzi zikiendelea vizuri, ununuzi wa samani na vifaa vya kufundishia na kujifunzia uko katika hatua ya kusaini mikataba.

Mpango wa kazi na uendeshaji wa kampasi mpya na mpango endelevu wa muda wa baada ya Mradi kukamilika umeandaliwa na kuidhinishwa na Baraza la Chuo kwa ajili ya utekelezaji. Chuo kinatambua kwamba uendelevu katika upatikanaji wa fedha ni jambo muhimu sana katika kuendelea kufaidi matokeo ya Mradi. Hivyo, Chuo kimedhamiria kuendelea kuwekeza katika ufundishaji, utafiti na ushauri wa kitaalamu.

Tunapoelekea kukamilisha shughuli za ujenzi na uzinduzi wa kampasi mpya, changamoto kama vile malazi kwa wafanyakazi na wanafunzi, huduma za kijamii kama vile mabenki, maduka na huduma za usafiri bado hazijatatuliwa.

Menejimenti ya Chuo inatumia fursa hii kuwahimiza wadau wetu kuzingatia changamoto hizo kama fursa kwenu, hivyo, kuwekeza katika maeneo hayo kama taasisi binafsi au kupitia mpango wa ubia kati ya sekta ya umma na binafsi.

Ninawakaribisha tena wasomaji wetu na ninatumai kwamba mtafurahia kusoma Jarida la Toleo la Nane.

# Ujumbe wa Mratibu



## Prof. Bernadeta Killian

### Mratibu wa HEET-UDSM

Ni wakati mwingine wa kufanya tafakuri na kuwaeleza wasomaji wetu hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa Mradi wa HEET, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mafanikio makubwa yamepatikana katika utekelezaji wa Mradi tangu tulipotoa taarifa mara ya mwisho.

Ujenzi unaoendelea katika maeneo ya Dar es Salaam, Zanzibar, Lindi na Kagera unaelekea kukamilika. Kazi nzuri imefanywa katika kufanikisha kukamilika kwa ujenzi huo.

Ununuzi na ufungaji wa samani katika majengo yote mapya uko katika hatua ya kusainiwa mkataba. Katika kipindi hiki, timu za wataalam zilifanya kazi ya kutathmini zabuni za ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Ni matumaini yetu kuwa mara baada ya kusainiwa kwa mikataba, ununuzi na ufungaji wa vifaa hivi utaanza ifikapo Disemba 2025. Tunafurahi kuwajuza kwamba uwekaji wa vifaa vya maltimedia katika kumbi za mihadhara zilizopo umekamilika tayari kwa matumizi kuanzia mwaka wa masomo wa 2025/2026.

Katika jitihada za kuboresha mitaala ambayo mbali na mambo mengine imezingatia matumizi ya mbinu bunifu, Seneti ya Chuo Kikuu imeidhinisha programu 248 (94 kutoka fani za kipaumbele na 154 kutoka katika fani nyingine). Kati ya programu zilizoidhinishwa na seneti, programu 237 zimewasilishwa TCU kwa ajili ya kuidhinishwa. Tunashukuru kwamba programu 32 (19 kutoka fani za kipaumbele) zimeidhinishwa na TCU.

Kwa upande wa mpango wa kukuza uwezo katika utafiti na ubunifu, mnamo mwezi Machi 2025, chuo kilifanya hafla ambapo wabunifu walipata fursa ya kuonesha kazi zao kwa wadau kwa lengo la kuonesha matokeo ya tafiti zao ili kuyabidhaisha.

Kuhusu uhusiano na wadau, Kamati za Ushauri wa Tasnia (IACs) zinaendelea kufanya mikutano ya mara kwa mara kama ilivyopangwa katika shajara, ambapo mikataba ya maridhiano 22 kati ya 25 imesainiwa kati ya UDSM na kampuni mbalimbali. Hadi sasa wafanyakazi wanataaluma na wale wa kiufundi 35 wameshiriki katika mafunzo ya uzoefu wa kazi za tasnia mbalimbali ambapo wengine 36 wanatarajiwa kushiriki ifikapo katikati ya Septemba 2025.

Kuhusiana na suala la kuimarisha matumizi ya teknolojia ya dijitali, shughuli nyingi zimekamilika huku nyingine zikiendelea. Kufikia mwezi Agosti 2025, zabuni zinazohusiana na ununuzi wa mtandao, vituo vya upatikanaji wa mtandao, masuala ya usalama na umeme wa dharula kwenye vifaa vya digitali zilikuwa katika hatua za mwisho zikisubiri kutolewa kwa barua ya zabuni. Kukamilika kwa shughuli za ununuzi wa mtandao ni pamoja na uwekaji wa mtandao wa data wa TEHAMA kutaimarisha matumizi ya teknolojia ya dijitali katika kufundishia na kujifunzia UDSM.

Uboreshaji wa mifumo ya Moodle LMS, Massive Open Online Courses (MOOC) na Open Education Resources (OER) umeongeza idadi ya watumiaji katika mifumo hiyo. Kwa mfano, idadi ya kozi zilizosajiliwa katika Moodle LMS imeongezeka kwa 180% kutoka 357 mwaka wa 2022 hadi kozi 1000 mwaka wa 2025.

Wakati huohuo Mfumo wa kidijitali wa UDSM wa Majarida ya Kitaaluma umekamilika kuanzia mwezi Desemba 2024. Idadi ya matoleo ya majarida yanayotolewa katika mfumo huu imeongezeka kwa 44% kutoka matoleo 25 mwezi Desemba 2024 hadi matoleo 36 mwezi Juni 2025.

Kwa upande wa taarifa kuhusu wafanyakazi wanataluma wanaondelea na masomo ya shahada za Uzamili nje ya nchi kwa ufadhili wa Mradi wa HEET, maendeleo yao yanaridhisha, ambapo wale waliohitimu masomo yao tayari wamerejea Chuoni wakiendelea na majukumu yao kama kawaida.

Chuo pia kimeendelea kufuatilia uzingatiaji wa utekelezaji wa Mradi kwa kutumia zana na mifumo mbalimbali. Ninafurahi kuripoti kwamba utekelezaji wa Mradi uko katika hatua za mwisho licha ya changamoto za hapa na pale. Kwa kuhitimisha, tunashukuru kwa ushirikiano tulioupata kutoka kwa wadau wetu ambao umechangia kupatikana kwa mafanikio yaliyoainishwa huku tukitaraji kuendelea kupata ushirikiano zaidi.

# Ujenzi wa Mradi wa HEET Wachochea Matumaini na Fursa Mpya Buyu - Zanzibar

*Na Zamda George, HEET-UDSM*



***Matokeo Chanya:*** *Jengo jipya la utawala na taaluma lililojengwa chini ya Mradi wa HEET katika Taasisi ya Sayansi za Bahari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (IMS), Buyu, Zanzibar, likiwa katika hatua za ukamilishaji, kama lilivyopigwa picha mwezi Septemba, 2025.*



***Ushirikiano:*** *Baadhi ya wakazi wa kata ya Itahwa, Bukoba, Mkoani Kagera, ambako Kampasi ya Kagera ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) inajengwa, wakishiriki katika kikao cha wadau pamoja na wataalamu wa Mradi wa HEET-UDSM kujadili maendeleo ya utekelezaji wa Mradi huo na uanzishaji wa kampasi hiyo mpya katika eneo lao.*

Wakati Mradi wa HEET ukikaribia kukamilika katika Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS) iliyopo Buyu, Zanzibar, wimbi la matumaini linazidi kutanda katika jamii inayozunguka eneo la Mradi.

Kwa mujibu wa Bi. Fatuma Juma, Mratibu wa Kamati za Kushughulikia Malalamiko (KASEMA) katika Mradi wa HEET-UDSM huko Buyu, tayari mabadiliko yanayotokana na Mradi yanaonekana. Pia, anaelezea namna ambavyo Mradi huu ulivyolibadilisha eneo la Buyu.

"Buyu inachangamka kutokana na ujenzi unaoendelea. Tumeshuhudia maduka mapya, vibanda vya chakula vya mamalishe, nyumba za kisasa na majengo ya biashara yakiongezeka kila uchao. Tunatarajia mabadiliko makubwa zaidi mara maabara mpya zitakapoanza kufanya kazi", alisema.

Maelezo yake yanaonesha namna Mradi wa HEET unavyoibadilisha Buyu na kuifanya kuwa kitovu cha ubora wa kitaaluma na maendeleo ya jamii.

Wavuvi kutoka katika eneo hilo pia wana matumaini makubwa. Bw. Faki Ali anaamini kuwa maabara mpya za IMS zitafungua milango katika masuala ya uvumbuzi ambayo yanayanufaisha moja kwa moja maisha yao. "Ni matumaini yetu kuwa utafiti na mafunzo yatakayotolewa kwa kutumia miundombinu hii yatasaidia katika kuibua teknolojia na uvumbuzi utakaosaidia kuimarisha shughuli zetu za uvuvi na hivyo kuboresha ustawi wa wavuvi wa Zanzibar".

Kupitia Mradi wa HEET, UDSM inajenga majengo mawili katika Taasisi ya Sayansi za Bahari - Zanzibar, moja jengo la utawala na shughuli za kitaaluma ikiwa ni pamoja na kumbi za mihadhara, maabara, ofisi, na ukumbi wa kisasa wa mikutano; jingine ni jengo la bweni la wanafunzi.

Majengo haya yanatarajia kuiongezea Taasisi uwezo wa kuchukua wanafunzi kutoka 88 hadi 216.

Manufaa tayari yameanza kuonekana kwa wakazi wanaozunguka eneo la Mradi. Maalim Kombo, mkazi wa muda mrefu wa Buyu, anasema Mradi huo utakuza Uchumi wa Bluu wa Zanzibar. "Maendeleo ya IMS Buyu ni ya Zanzibar yote. Maabara hizi zitatusaidia kuboresha shughuli za kilimo na hivyo kufanikisha malengo ya kuelekea katika ukuaji endelevu wa Uchumi wa Bluu.

Manufaa yanaonekana pia katika huduma za usafiri na usafirishaji. Akitoa ushuhuda kuhusu manufaa haya dereva mmoja wa bodaboda ndugu Ahmed Mfaume anasema: "Kila wakati ninapopeleka abiria kwenda Buyu, naona mabadiliko mapya: barabara zinaboreshwa, majengo mapya yanaongezeka, na idadi ya safari kwenye njia hii pia imeongezeka sana kutokana na miradi inayoendelea".

IMS iko katika maandalizi ya kuzindua awamu yake ya pili majengo yake ya kisasa yenye ofisi, kumbi za mikutano na maabara na hivyo kuendelea kuisisimua jamii. Kuanzia kuwa na eneo lenye biashara ndogondogo na huduma duni za usafiri hadi kuwa na ubunifu wa hali ya juu katika shughuli za uvuvi na Uchumi wa Bluu ambapo manufaa haya yatayanufaisha pia maeneo mbalimbali ya Zanzibar.

IMS haiuangazii Mradi wa HEET katika maendeleo ya kitaaluma pekee, bali pia inautazama Mradi kama kichocheo cha mabadiliko ya jamii ambapo sayansi na uvumbuzi vinaenda sambamba na uboreshaji wa maisha ya jamii.

# Mpango wa Kujenga Uwezo Wakuza Viwango vya Kitaaluma na Utendaji UDSM

*Na Renancy Remmy na Donald Boneka, HEET-UDSM*




**Bw. Gabriel Mwaijande Paul**
Mhitimu wa Shahada ya Umahiri ya Sayansi katika Uhandisi wa Jiotekniki, Chuo Kikuu cha Leeds, Uingereza



**Bi. Angelina William**
Mhitimu wa Shahada ya Umahiri ya Sayansi katika Sayansi ya Chakula, Chuo Kikuu cha Reading, Uingereza

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimeboresha kiwango cha kitaaluma na uwezo wake katika kufanya uamuzi wa kitaasisi kupitia Mpango wake wa Kujenga Uwezo uliofadhiliwa na Mradi wa HEET.

Mpango huo umepata mafanikio makubwa katika uboreshaji wa mitaala na mageuzi ya kitaaluma kupitia mapitio ya mitaala yaliyofanywa kwa ufanisi wa hali ya juu. Jitihada hizi zinalenga kuimarisha utendaji wa kitaasisi, uendelevu, na ubora wa kitaaluma kimataifa.

Kwa mujibu wa Dkt. Emmanuel Stephen Matee, mtaalamu wa kujenga uwezo wa Mradi wa HEET-UDSM, mpango umeandaliwa kwa kuzingatia jitihada za makusudi na zilizoandaliwa mahususi kwa lengo la kuongeza ujuzi, umahiri na mifumo ya kitaasisi.

"UDSM imekwishatoa ufadhili wa masomo kwa wanataaluma 29 katika programu za Uzamivu na Umahiri katika vyuo vikuu vya kiwango cha kimataifa kama sehemu ya mpango huu wa muda mrefu", alisema Dkt Matee.

Aliongeza kuwa: "Wanataaluma wengi waliokuwa wakisoma Shahada ya Umahiri tayari wamekwishahitimu, na wengine wako mbioni kuhitimu masomo yao. Wahitimu waliorejea na watakaorejea wataendelea kuiimarisha UDSM kwa njia ya ufundishaji na utafiti kwa kuzingatia mitaala iliyoboreshwa".

Dkt. Matee alieleza kuwa shughuli zilizolengwa kufanywa katika mpango wa muda mfupi zimenufaisha kundi kubwa la watumishi wa UDSM, wakiwamo viongozi waandamizi, wafanyakazi wa kada ya kiufundi, na wanataaluma chipukizi.

"Mipango muhimu ilijumuisha mafunzo ya muda mfupi, ziara za ulinganishiviwango kwa viongozi, ambapo viongozi waandamizi wa UDSM walitembelea vyuo vikuu maarufu duniani ili kujifunza mbinu bora za utawala, ushirikiano wa masuala ya kifedha, na ubunifu katika masuala ya kitaaluma", alisema.

Prof. Nelson Boniface, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo, Utafiti, alisisitiza dhamira ya Chuo katika kuendeleza rasilimaliwatu na mifumo ya kitaasisi. "Katika kujenga uwezo, Chuo kimewekeza kwa watu wake na mifumo ili kuinufaisha jamii ya ndani na nje ya UDSM. Wahitimu wetu, matokeo ya utafiti, na ushirikiano tunaofanya kwa pamoja vitanufaisha moja kwa moja tasnia mbalimbali, wanajamii, na kuchangia katika uboreshaji wa sera".

Alisisitiza zaidi kwamba lengo la UDSM ni kuendeleza mafanikio haya kupitia maendeleo endelevu ya kitaaluma, kukuza mnyororo wa mfumo wa ubunifu, na ujenzi wa mifumo thabiti ya masuala ya kitaaluma.

"UDSM imejikita katika kuendeleza mafanikio haya kwa kujikita katika maendeleo endelevu ya kitaaluma, kukuza mifumo ya ubunifu, na kujenga miundo thabiti ya kitaaluma. Chuo kimedhamiria kuwa mstari wa mbele sio tu katika kuleta mabadiliko ya elimu ya juu, bali pia katika kutatua changamoto zinazoikabili jamii kama vile ukosefu wa ajira, tofauti za kijinsia na changamoto za kiteknolojia," Ameongeza.

"Lengo kuu ni kuhakikisha kwamba Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinabaki kuwa kinara katika utoaji wa elimu ya juu barani Afrika, kuchochea mabadiliko ambayo yanajitokeza kitaifa, kikanda na kimataifa," Ameendelea kueleza.

Wakati huo huo, Prof. Donatha Tibuhwa, Mkurugenzi wa Udhibiti Ubora UDSM, akiangazia matokeo yanayoonekana ya afua za kujenga uwezo alisema: "Mafunzo hayo yamewawezesha viongozi wetu waandamizi na wanataaluma kufikiri kimkakati na kuwa na utendaji thabiti. Hivi sasa tumejiimarisha katika kuboresha mitaala, kukuza ushirikiano baina ya vitengo na uzingativu endelevu wa masuala ya udhibiti ubora".

### *Kuweka Viwango katika Ubora wa Kitaaluma*

Dkt. Matee pia alibainisha kuwa mpango huo wa kuwajengea uwezo umeisaidia UDSM kuweka viwango vipya katika ubora wa kitaaluma na maendeleo ya taasisi.

*Inaendelea Uk. 7...*

...inatoka Uk. 6

"Katika jitihada za kujenga uwezo, UDSM imekuwa ikiweka vigezo vipya katika ubora wa kitaaluma na ukuaji wa kitaasisi kupitia mipango madhubuti ambayo imewekwa kimkakati ili kuendana na mwelekeo wa elimu ya juu duniani huku ikishughulikia vipaumbele vya maendeleo ya Tanzania na mahitaji ya rasilimaliwatu duniani," alisema Dkt. Matee.

Kujenga uwezo kunawakilisha njia ya kimageuzi inayoimarisha masuala ya utawala, ufundishaji, utafiti, ubunifu, na utoaji wa huduma kwa viwango vipya. Mpango huu ni sehemu muhimu ya mkakati wa muda mrefu wa UDSM wa kuendelea kuwa kinara katika masuala ya ufundishaji na ubunifu barani Afrika.

"Tunapojiimarisha katika maendeleo ya watu na miundombinu, tunaziba pengo la taaluma na mahitaji ya tasnia huku tukihakikisha kuwa kunakuwa na uendelevu hata baada ya kumalizika kwa muda wa Mradi wa HEET", alisema.

Aliendelea kueleza kwamba mitaala mbalimbali inayo endana na mahitaji soko la dunia imeandaliwa chini ya Mradi wa HEET kwa lengo la kushughulikia mahitaji ya sasa na ya baadaye ya soko la ajira.

"Hata hivyo, ili kutekeleza mtaala huo kwa ufanisi, UDSM inazingatia umuhimu wa kuwa na watumishi wenye ujuzi wa hali ya juu na vitendeakazi vya kisasa. Hali hii imesababisha kuandaliwa kwa mfumo madhubuti unaojikita katika mipango ya muda mrefu na muda mfupi, alisema Dkt. Matee.

Vilevile, warsha maalumu zimefanyika kuhusu masuala ya jinsia, ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu, usimamizi wa wanafunzi wa uzamili, uwianishaji wa majukumu ya kitaaluma na kiutawala kwa wanawake wenye majukumu ya uongozi, na uendelezaji wa ujuzi. Warsha hizi zimelenga kuongeza ujuzi kwa wafanyakazi wa maabara na karakana kwa kuzingatia viwango vya teknolojia ya kisasa.

"Mipango hii imewapa wafanyakazi wetu ujuzi na maarifa mahususi, kama vile fikra za kimkakati, maarifa kuhusiana na masuala ya kidijitali, na ujuzi wa uongozi, ambao ni muhimu kwa ufanisi wa mitaala iliyoboreshwa na maendeleo ya UDSM kwa ujumla," alisema Dkt. Matee.

Mkurugenzi wa Huduma za Jamii ambaye pia ni Mratibu wa Masuala ya Jinsia katika Mradi wa HEET-UDSM Dkt. Lulu Mahai, alipongeza namna ambavyo mitaala ilivyozingatia suala la ufanisi katika utoaji wa huduma. Hali hii inayodhihirisha uzingativu wa utoaji wa fursa kwa wote inadhihirisha moja kwa moja dhamira ya Chuo Kikuu ya kuzingatia mahitaji ya wanafunzi wote na ushindani wa kimataifa".



*Uongozi wa Kimkakati: Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ndugu Xavier Daud (katikati- waliokaa) akiwa na baadhi ya viongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo, Mhe. Balozi Mwanaidi Sinare Maajar (wa tatu kulia-waliokaa) na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye (wa tatu kushoto-waliokaa) mara baada ya Naibu Katibu Mkuu kufungua semina ya viongozi wa UDSM iliyofanyika katika Shule ya Uongozi, Kibaha, Pwani, mwezi Juni, 2025.*



**Dkt. Emmanuel Matee**,
Mtaalamu wa Kujenga uwezo wa Mradi wa HEET,
Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Programu imeandaliwa kimkakati ili kuongeza manufaa ya kitaasisi. Walengwa wakuu ni pamoja na viongozi waandamizi wa UDSM, marasi, maamidi, wakurugenzi, wakuu wa idara kuu, wafanyakazi chipukizi katika kada ya wanataaluma na ile ya kiufundi, wanawake wanataaluma wenye majukumu ya kiutawala, na wasimamizi wa Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi wa HEET.

Njia zilizotumika ni pamoja na ziara ya ulinganishiviwango, vipindi rasmi vya mafunzo, na uambatizi katika tasnia mbalimbali ambao umehusisha kuwianisha maarifa yaliyopo ya kitaaluma na mahitaji halisi ya jamii.

Mpango wa kujenga uwezo tayari umeanza kutoa matokeo yanayoweza kupimika. Hii ni pamoja na kuboreshwa kwa maamuzi ya kimkakati, uimarishaji wa ushirikiano katika vitengo vya kitaaluma na kiutawala, kuongezeka kwa uwajibikaji, mbinu bunifu za ufundishaji na utawala, na uendelevu matokeo ya Mradi wa HEET.

Wadau wa kutoka kundi la wanajumuiya na jamii inayozunguka eneo la Mradi pia wameanza kushuhudia manufaa hayo.

Mwanajumuiya mmoja kutoka katika Idara ya Uhandisi wa Umeme Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia, ambaye amehitimu masomo yake nje ya nchi hivi karibuni, alikuwa na haya ya kusema: "Mafunzo niliyoyapata kimsingi yamenijengea uwezo wa kufanya mageuzi katika mbinu za ufundishaji na kufanya utafiti. Sasa ninahusisha zaidi mbinu za kiutendaji na uunganishaji wa maarifa na utendaji halisi katika tasnia mbalimbali ambapo wanafunzi wangu wanahisi kushirikishwa ipasavyo.

Mfano huu unadhihirisha kwamba juhudi za kujenga uwezo kupitia Mradi wa HEET sio tu kwamba zinawanufaisha wafanyakazi na wanachuo bali pia zinainufaisha jamii pana kwa kutoa wahitimu wenye uwezo zaidi na kuwa na tafiti zenye matokeo chanya.

Mpango huu wa kujenga uwezo wa UDSM unachangia katika jitihada zinazoendelea za mageuzi ya elimu ya juu nchini Tanzania na kusaidia katika utekelezaji wa ajenda ya kitaifa ya kuwa na watumishi wenye ujuzi ambayo pia inawiana na utekelezaji wa Dira ya 2050 na Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Katika ngazi ya kimataifa, UDSM inatazamwa kama mshirika muhimu na wa kuaminika katika ushirikiano wa kimataifa katika masuala ya ufundishaji na utafiti.

Kwa kuzingatia maendeleo ya rasilimaliwatu na mifumo ya kitaasisi, Mpango wa Kujenga Uwezo wa kupitia Mradi wa HEET unaisaidia UDSM kuwa kichocheo katika kuleta mabadiliko katika elimu ya juu, ndani na nje ya nchi.

# Mapitio ya Mtaala Yafikia Hatua ya Mwisho, Programu Mpya 32 zapata Ithibati

***Na Ally Mambele, HEET-UDSM***



***Mwelekeo Sahihi:*** *Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambaye pia ni Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete (katikati), akitoa maelezo alipotembelea vijiji vya Itahwa na Kangabusharo ambako ndiko kampasi mpya ya UDSM Kagera ilipojengwa. Mkuu wa chuo aliongozana na viongozi na watumishi wengine wa UDSM wakiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye (kulia-mstari wa mbele).*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinakaribia kukamilisha mpango wake wa kihistoria wa mapitio ya mitaala ikiwa ni miongoni mwa vipengele muhimu katika Mradi wa HEET.

Katika mahojiano maalum na jarida hili, Dkt. Geradius Kikumi, Mratibu kutoka Kurugenzi ya Masomo ya Shahada za Awali, UDSM, alibainisha maendeleo makubwa yaliyofikiwa na kudokeza kuwa takriban programu zote zilizokusudiwa kupitiwa zimepitiwa na kuwasilishwa katika mamlaka husika ambapo nyingi tayari zimekwisha idhinishwa.

"Mwamko katika mapitio haya ya mitaala ni mkubwa sana. Tuko katika hatua za mwisho za mchakato ambao utafafanua upya ubora wa kitaaluma katika UDSM. Tumefanikiwa kuwasilisha programu 239, kati ya programu 250 zilizopangwa kuwasilishwa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kwa ajili ya kuridhiwa na kupata ithibati kwa ngazi zote za shahada ya awali na uzamili", alisema Dkt. Kikumi.

Ameendelea kueleza kwamba TCU imeidhinisha rasmi na kutoa ithibati kwa programu 32 kwa ajili ya kuanza kutumika katika mwaka wa masomo 2025/2026. "Hatua hii inadhihirisha matokeo ya awamu ya kwanza ya mapitio ya mitaala ya kisasa yaliyolenga kuandaa viongozi na wabunifu kwa kizazi kijacho".

Aliongeza: "Kipengele muhimu kilichozingatiwa katika mapitio haya ni matumizi ya teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji. Takriban 40% ya programu zilizoidhinishwa zimezingatia matumizi ya mkabala mseto katika ufundishaji na ujifunzaji ambao unahusisha ufundishaji wa ana kwa ana na matumizi ya teknolojia. Mkabala huu unalenga kuimarisha matumizi ya zana zilizopo huku ukizingatia ubora wa kitaaluma".

Dkt. Kikumi alibainisha kuwa, miongoni mwa programu zilizoidhinishwa, ni Digrii ya Awali ya Sayansi katika Fizikia (Fizikia tiba) ambayo inatazamwa kama miongoni mwa programu muhimu sana.

"Programu hii ni uthibitisho wa dhamira ya UDSM ya kushughulikia maeneo muhimu yenye athari kubwa kwa jamii. Wahitimu wanatarajiwa kuwa na utaalamu katika matumizi ya teknolojia za kisasa za upigaji picha na tiba ya mionzi na hivyo kuchangia moja kwa moja katika kuboresha sekta ya afya nchini Tanzania na kote Afrika", alisema.

Naye Prof. Masoud Muruke, Mratibu wa Mapitio ya Mtaala katika Mradi wa HEET-UDSM alisema kuwa mchakato huo, ambao ufanisi wake unaonyesha dhamira ya Chuo Kikuu katika kuboresha utoaji wake wa kitaaluma na kuandaa wahitimu wanaoendana na mahitaji ya soko la ajira, ulizingatia vipengele muhimu vinavyolenga kuimarisha ubora na umuhimu wa programu za kitaaluma zinazotolewa na UDSM.

"Mchakato wa mapitio ya mtaala sio tu kwamba umehusisha kupitia na kuboresha kozi kama ilivyozoeleka bali umehusisha pia kufanya mageuzi ya namna ya kuwaandaa wahitimu wetu ili kuendana na mahitaji ya sasa ya ulimwengu unaobadilika kwa kasi. Tunahakikisha kwamba wahitimu wetu wanapata maarifa na ujuzi sahihi kwa ustawi", alisema Prof. Muruke.

Pia, alisema kuwa mapitio ya mitaala yalianza kwa tathmini ya kina ya programu zilizopo. Aidha, watahini wa ndani na wa nje, wadau kutoka katika tasnia mbalimbali walitoa maoni muhimu ikiwa ni pamoja kubainisha maeneo yanayohitaji kuboreshwa.

Mchakato huo uliimarishwa zaidi kwa kufanya ziara ya ulinganishiviwango katika taasisi maarufu nchini Afrika Kusini, Ghana, Korea Kusini, Ujerumani na Malaysia. Ziara hizi ziliongeza maarifa muhimu katika mbinu bora za kimataifa katika uandaaji na usimamizi wa mtaala.

Kuidhinishwa kwa mafanikio kwa programu hizi ni alama ya mafanikio muhimu kwa Mradi wa HEET, kuimarisha jukumu la UDSM kuwa kinara katika ubunifu na mageuzi ya kiuchumi. Wanajumuiya sasa wana hamu ya kuona programu za kisasa zikianza kufundishwa katika mwaka wa masomo wa 2025/2026.



***Furaha Kubwa:*** *Baadhi ya wahitimu wa Mahafali ya 53 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiwa na furaha wakati wa maandamano ya kitaaluma katika mahafali iliyofanyika mwezi Novemba, 2023 katika Ukumbi wa Mlimani City .*

# Programu ya Uambatishaji Wafanyakazi wa UDSM Kwenye Tasnia Yabadilisha Mtazamo wa Kitaaluma

*Na Zamda George, HEET-UDSM*



***Dira ya Mageuzi:*** *Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Utafiti, Prof. Nelson Boniface (wa kwanza kulia) akiongoza kikao cha nne cha Kamati ya Ushauri wa Kitasnia upande wa Insia, Sayansi za Jamii, na Usimamizi wa Rasilimali, kilichofanyika hivi karibuni, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*



***Kwa Vitendo:*** *Bi. Catherine James (kushoto), mtumishi kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET), akishiriki katika programu ya uambatishaji watumishi akijikita katika uwekaji rangi kwenye vitambaa katika kiwanda cha Sunflag Tanzania Ltd, Arusha, Aprili 2025. Pembeni yake ni mtumishi wa kiwanda hicho.*

Wahadhiri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) wamesifu awamu ya pili ya Programu ya Uambatishaji Wafanyakazi wa Chuo Kikuu ambayo imewawezesha kuwa na uzoefu wa kimageuzi, unaotoa mwelekeo wa taaluma zao.

Jitihada hizi, ambazo ni sehemu ya Mradi wa HEET, zimebuniwa kimkakati ili kuimarisha uhusiano kati ya taaluma na tasnia husiani kwa kuwazamisha wanataaluma katika mazingira halisi ya kitaaluma na kikazi.

Uambatishaji huu umezihusisha sekta mbalimbali ambazo ni pamoja na mafuta na nishati, nguo, TEHAMA, ufugaji wa viumbe maji na usafirishaji. Programu hii inashughulikia moja kwa moja pengo lililopo kati ya maarifa ya kinadharia na matumizi yake katika tasnia muhimu za uchumi wa Tanzania.

Miongoni mwa washiriki wa mwaka huu ni Dkt. Rachel Sabuni, mhadhiri katika Taasisi ya Sayansi za Bahari, Zanzibar (IMS). Uambatishwaji wake katika Kiwanda cha Gesi cha Songo Songo mkoani Lindi ulimpa mtazamo wa kipekee kuhusu uendeshaji wa gesi na mfumo wa udhibiti nchini Tanzania, akifanya kazi kwa karibu na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) pamoja na uongozi wa kiwanda.

"Programu hii imenipa uelewa wa moja kwa moja kuhusu shughuli za usimamizi na udhibiti wa gesi. Ni uzoefu wa thamani ambao nina shauku ya kuwashirikisha wanafunzi wangu. Kushuhudia shughuli hizi kwa karibu kumeupanua mtazamo yangu, na ninatarajia kuwahamasisha wahandisi wa kizazi kijacho kwa kutumia maarifa haya niliyoyapata kwa vitendo," alisema Dkt. Sabuni.

Programu hii iliungwa mkono kikamilifu na PURA, mshirika muhimu wa Mradi wa HEET aliyejitolea kuongeza uwezo wa udhibiti kupitia ushirikiano wa kielimu. Bw. Leonard Ndau, mhandisi wa petroli katika PURA, alisifu jitihada hizi: "Programu ya Uambatishaji Wafanyakazi wa UDSM ni jitihada ya kupongezwa inayounganisha kwa ufanisi maarifa ya kitaaluma na vitendo."

Alisisitiza manufaa ya pande zote mbili: wafanyakazi wa UDSM wanapata uelewa halisi wa kazi, huku PURA ikifaidika na mitazamo mipya ya kitaaluma. "Jitihada hizi zimeweka msingi thabiti wa ushirikiano madhubuti zaidi kati ya PURA na UDSM. Tukishirikiana kwa karibu, tunaweza kuhakikisha kuwa ufundishaji na utafiti vinaendelea kuendana na mahitaji ya tasnia na taifa kwa ujumla."

Aidha, Bw. Ndau alisifu taaluma na weledi ulioonešhwa na wahadhiri wa UDSM katika mijadala ya kiufundi na ya udhibiti, akipendekeza kwamba kwa siku zijazo uambatishaji kwa muda mrefu zaidi unaweza kuleta matokeo makubwa zaidi.

### *Sekta Tofauti, Mafunzo kwa Vitendo*

Wigo wa programu hii ulienda mbali zaidi ya mafuta na gesi, ambapo wanataaluma kutoka UDSM walipata uzoefu wa moja kwa moja katika sekta mbalimbali. Katika sekta ya nishati, Bi. Heavenlight Munisi kutoka Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET) alijiunga na timu za uwandani katika Kampuni ya Pivotech, akihawilisha utaalamu wake wa uhandisi kwa vitendo katika matengenezo na ukarabati wa majenereta.

Katika teknolojia ya magari, Bw. Lusajo Mwamakula kutoka CoET alifanya kazi na Wakala wa Ufundi wa Umeme Tanzania (TEMESA), Kigoma, akijifunza mbinu muhimu za ukarabati wa magari kama kusugua, kujaza na kupaka rangi.

Kwa upande wa sekta ya nguo, Bi. Catherine James kutoka CoET alijikita katika uchakataji wa rangi za nguo na uendelevu katika kiwanda cha Sunflag Tanzania Ltd Arusha, huku wenzake wakichunguza mbinu za kurejeleza majitaka na taratibu za udhibiti wa ubora.

Kwa upande wa sekta ya TEHAMA, Dkt. Godwin Gadiel kutoka Ndaki yaTeknolojia ya Habari na Mawasiliano

*Inaendelea Uk. 26...*

# Mfumo wa Ushughulikiaji Malalamiko Wafanikisha Uzingatiaji Madhubuti wa Taratibu katika Utekelezaji wa Mradi wa HEET

***Na Jackson Isdory, HEET-UDSM***



***Ushirikishwaji wa Jamii:*** *Dkt. Armstrong Matogwa, mjumbe wa Kamati ya HEET-UDSM- ya Ufuatiliaji, Tathmini na Mafunzo yaliyopatikana, akionesha zana za Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko kwa wakazi wa Ngongo, katika eneo la Mradi wa HEET UDSM mwaka 2024.*



***Ulinzi na Usalama:*** *Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Mipango, Fedha na Utawala ambaye pia ni Mratibu wa Mradi wa HEET, Prof. Bernadeta Killian (wa pili kushoto) pamoja na Naibu Mratibu wa HEET, Prof. Liberato Haule, wakiwa kwenye kikao na wajumbe wa Kamati ya Kushughulikia Malalamiko katika eneo la Mradi wa UDSM-HEET Lindi, mwaka 2024.*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimeimarisha mfumo wa uzingatiaji wa taratibu katika utekelezaji wa Mradi kupitia mafanikio ya utekelezaji wa Kamati za Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko chini ya Mradi wa HEET.

Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye, alisema kuwa Mfumo huo umekuwa na mchango mkubwa katika kukuza imani, uwajibikaji katika utekelezaji wa Mradi na ushirikishwaji wa jamii.

“Kama Chuo Kikuu, tuna dhamana ya kimaadili na kitaasisi ya kuhakikisha maendeleo ni jumuishi, yenye uwazi na endelevu. Mfumo huu umeakisi dhamira hii kwa kuwapa wadau wote kuanzia maafisa wa serikali hadi wananchi fursa ya kuchangia kufanikisha mustakabali wa elimu ya juu. Nafasi ya Mfumo katika kukuza imani na uwajibikaji imewasaidia wadau kuhisi kuwa wako salama na kuwa na imani na usimamizi wa Mradi,” alisema Prof. Anangisye.

Ufadhili wa Mradi wa HEET unatolewa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushirikiana na Benki ya Dunia, ukiwa na lengo la kufanya mageuzi katika elimu ya juu ili kukidhi mahitaji ya kitaifa ya maendeleo ya kiuchumi na kikanda yanayoongezeka kila uchao. Mradi huu unalenga zaidi ujenzi na uendelezaji wa miundombinu, utafiti, ubunifu, na kujenga uwezo.

Dkt. Edmund Mabhuye, Mtaalamu wa Maendeleo ya Mazingira wa Mradi wa HEET-UDSM, alisema kuwa kutokana na shughuli za Mradi kuenea katika maeneo mbalimbali nchini, Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko umekuwa nyenzo muhimu ya kutatua malalamiko, kukuza uwajibikaji, na kulinda uendelevu wa matokeo.

“Maeneo haya si tu kwamba yanatumia mifumo inayojumuisha kanuni za mazingira, kijamii na kiutawala, bali pia yameleta mageuzi chanya katika jamii za wenyeji,” alisema Dkt. Mabhuye.

Aliendelea kueleza kuwa maeneo hayo yamejumuisha kanuni mahususi za mazingira, kijamii na kiutawala, kama vile matumizi ya mbinu endelevu za ujenzi, maendeleo ya kijamii, na taratibu za ajira zinazozingatia haki. Vipengele muhimu vya mafanikio vinajumuisha ushirikishwaji; utatuzi wa migogoro kwa wakati; uzingatiaji wa tofauti za kitamaduni; na mfumo wa wazi wa kutoa mrejesho. Vipengele hivi kwa pamoja vinakuza umiliki wa pamoja miongoni mwa wadau na kuboresha utoaji wa huduma.

Kupitia Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko, maeneo haya yana mifumo ya uzingatiaji taratibu inayoendana na viwango vya mazingira, kijamii na kiutawala. Mifumo hii inasaidia maendeleo endelevu ya miundombinu huku ikipunguza vihatarishi vya uendeshaji.

Manufaa makuu ya muda mrefu yanajumuisha kuboreshwa kwa usimamizi wa miundombinu; kuimarishwa kwa miundombinu ya kitaaluma; kuongezeka kwa uwezo wa kitaaluma na utafiti; kupungua kwa uharibifu wa mazingira

*Inaendelea Uk. 24...*



***Ushirikishwaji Wadau:*** *Ubainishaji na Mafunzo kuhusu Ukatili wa Kijinsia kwa watoa huduma katika maeneo mbalimbali ya ujenzi wa Mradi wa HEET UDSM nchini Tanzania chini ya Mratibu wa masuala ya Jinsia wa Mradi wa HEET-UDSM na Mkurugenzi wa Taasisi ya Jinsia, Dkt. Lulu Mahai (kushoto-aliyesimama).*

# UDSM Yaongoza Mradi wa HEET Ukikamilika kwa 74% Kitaifa

*Na Wilson Remmy, HEET-UDSM*



***Mwanzo Mpya:*** *Jengo jipya la biashara lililojengwa chini ya Mradi wa HEET, lenye maeneo ya mgahawa, huduma za benki na nyinginezo katika Kampasi ya UDSM Kagera*

Mradi wa HEET uko katika nafasi ya kubadilisha kabisa mazingira ya elimu ya juu nchini Tanzania, baada ya kufanikisha utekelezaji kwa asilimia 74 kitaifa. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kipo mstari wa mbele katika utekelezaji huu, kikiripoti maendeleo ya kipekee Mradi huu unapoelekea mwishoni mwezi Julai, 2026.

Taarifa hii ilitangazwa katika Mkutano wa Kitaifa wa Waratibu uliofanyika UDSM kuanzia Septemba 15–18, 2025. Mratibu wa Kitaifa wa Mradi, Dkt. Kennedy Hosea, alisifu hatua hiyo kuwa ni ushahidi wa utekelezaji wa kimkakati na dhamira madhubuti kutoka taasisi zote zinazoshiriki.

"Ufikwaji wa hatua hii muhimu unaonesha si tu upangaji makini bali pia kujitolea kwa dhati kwa taasisi zetu zote zinazotekeleza Mradi huu. Tumejizatiti kikamilifu kuhakikisha kuwa tunakamilisha Mradi huu wa mageuzi kwa wakati," alisema Dkt. Hosea.

Akimwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Utafiti, Prof. Nelson Boniface, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano. "Jukwaa hili ni muhimu kwa lengo la kubadilishana mbinu bora za utekelezaji Mradi, kuimarisha ushikamano, na kuhakikisha kuwa Mradi unafanikisha kikamilifu malengo yake ya kitaifa".



***Ulimwengu wa Dijitali:*** *Baadhi ya viongozi na watumishi wa UDSM baada ya uzinduzi wa mafunzo ya kujenga uwezo wa utoaji wa programu za mafunzo kwa njia ya mtandao na njia mseto, yaliyofanyika katika Ukumbi wa Maktaba ya UDSM tarehe 6 Oktoba, 2025.*



***Matumaini Thabiti:*** *Mratibu wa Kitaifa wa Mradi wa HEET, Dkt. Kennedy Hosea, akizungumza katika kikao cha waratibu wa Mradi kilichofanyika hivi karibuni mwezi Septemba, 2025 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

Mkutano huo uliwakutanisha waratibu wa miradi, wataalamu wa kiufundi, na wataalamu wa masuala ya ufuatiliaji, TEHAMA, utunzaji wa mazingira, tasnia husiani, pamoja na mawasiliano kutoka kote nchini.

### *UDSM Yaongoza Utekelezaji wa Mradi kwa Asilimia 80*

Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM, Prof. Liberato Haule, ameripoti kuwa chuo kimevuka wastani wa kitaifa kwa kufanikisha utekelezaji wa asilimia 80 kufikia Agosti 2025. Mafanikio haya yanaonekana katika kampasi mbalimbali ikiwamo Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani, Taasisi ya Sayansi za Bahari Zanzibar, pamoja na kampasi mpya zilizoko Lindi na Kagera.

Mradi huu umechochea mageuzi makubwa ya miundombinu na mifumo ya kidijitali. "Tumekarabati na kujenga kumbi mpya za mihadhara, studio, karakana na maabara, kuboresha mabweni ya wanafunzi, na kwa kiasi kikubwa kuongeza miundombinu rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum," alifafanua Prof.Haule.

Mbali na miundombinu, Mradi huu unahakikisha kuwa programu za kitaaluma zinaendana moja kwa moja na mahitaji ya kijamii na kiuchumi. "Wataalamu kutoka tasnia husiani wamekuwa kiungo muhimu katika kuboresha mitaala yetu. Kupitia fuatilizi tumepitia upya, kufuta na kuanzisha programu mapya ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira, na kufanikisha zaidi ya programu 20 sasa kufundishwa kwa njia ya mtandao," aliongeza

Prof. Haule pia alibainisha dira ya muda mrefu ya UDSM, akieleza utekelezaji wa Mpango wa Miaka Kumi wa kuwa na Kampasi Maizi unaolenga kuunganisha teknolojia katika shughuli zote za kitaaluma na kiutawala.

*Inaendelea Uk. 12...*

...inatoka Uk. 11

### *Mpango wa Uendelevu na Mafanikio*

Kuhusu uendelevu, Prof. Haule alisisitiza kuwa mpango umeandaliwa ili kuhakikisha kuwa matokeo ya Mradi wa HEET yanakuwa endelevu hata baada ya Mradi kukamilika. “Mpango wetu jumuishi wa uendelevu unahusisha miundombinu, maboresho ya mitaala, mifumo ya dijitali, kujenga uwezo, usawa wa kijinsia, na programu za mazingira. Mpango huu tayari umeridhiwa katika ngazi mbalimbali za uongozi wa chuo na unasubiri kuidhinishwa rasmi na Baraza la Chuo,” ameeleza Prof. haule.

“Jambo la msingi la kuzingatia ni kuwa UDSM imefanikiwa kwa asilimia 100 kutimiza malengo yake makuu ya Mradi. Lengo la kwanza lilihusu uambatishaji wa wanafunzi na wanataaluma, ambapo tulilenga jumla ya watu 1,369 lakini lengo limetekelezwa zaidi ya iliyopangwa kwa kufanikiwa kuambatisha watu 4,719,” alisema Prof. Haule.

Aliongeza kuwa lengo la pili lilihitaji kupitiwa kwa programu 60 ili ziendane na mahitaji ya soko la ajira, na lengo hilo limekamilika kikamilifu. Pia, lengo la tatu lililolenga wanafunzi 23,162 kunufaika moja kwa moja na hatua za Mradi pia limefanikiwa kikamilifu,”

Mradi wa HEET ulizinduliwa mwaka 2022 kwa ufadhili wa Dola za Kimarekani milioni 425 (takribani Shilingi za Tanzania bilioni 972),kutoka Benki ya Dunia ukiwa na muda wa miaka mitano wa utekelezaji kwa lengo la kuboresha mfumo wa elimu ya juu nchini Tanzania. UDSM imepata mgawo wa Dola za Kimarekani milioni 49.5.

### *Kutoa taarifa ya Mageuzi ya Kitaifa*

Dkt. Hosea aliipongeza UDSM kwa jitihada zake za dhati katika kuufahamisha umma kuhusu manufaa ya Mradi na kuzitaka taasisi nyingine kuongeza nguvu katika kufikisha taarifa hizo. “Mradi wa HEET ni nguzo kuu ya maendeleo ya taifa kijamii na kiuchumi. Ni muhimu sana kuzieleza taarifa hizi za mafanikio kwa upana,” alisema Dkt. Hosea

Akifafanua mkakati wa UDSM, Dkt. Dotto Paul Kuhenga, Mkuu wa Mawasiliano na Masoko UDSM, na Mtaalamu wa Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano wa Mradi wa HEET-UDSM, alieleza mbinu jumuishi zinazotumika.

“Tumefanikisha upatikanaji mkubwa wa habari kupitia vyombo vya habari, tumekuwa tukitoa jarida mara kwa mara, kuandaa maandiko ya uhamasishaji, na kusimamia kwa ufanisi mitandao ya kijamii pamoja na tovuti mahususi ya Mradi. Ziara katika maaeneo ya utekelezaji wa Meadi na matukio muhimu vinalenga kuhakikisha kwamba taarifa za mageuzi kupitia Mradi wa HEET zinajumuishwa ipasavyo”, alisema Dkt. Kuhenga.

Kupitia jitihada hizi za pamoja, UDSM inaendelea kuthibitisha nafasi kuu ya Mradi wa HEET katika kujenga mfumo wa elimu ya juu unaoendana mahitaji ya sasa na ya baadaye katika kukuza maarifa madhubuti kwa uchumi wa Tanzania.



*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano na Masoko cha UDSM, ambaye pia ni mtaalamu wa Mawasiliano ya Umma kwa Mradi wa HEET, Dkt. Dotto Paul Kuhenga, akizungumza katika kikao cha waratibu wa Mradi kilichofanyika hivi karibuni mwezi Septemba, 2025 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*




*Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET, Prof. Liberato Haule, akizungumza katika kikao cha waratibu wa Mradi kilichofanyika hivi karibuni mwezi Septemba, 2025 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*



***Matumaini:*** *Washiriki wa kikao cha waratibu wa Mradi wa HEET kilichofanyika hivi karibuni mwezi Septemba, 2025 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

# Vifaa vya Kisasa Vyabadili Elimu ya Wenye Mahitaji Maalum UDSM

***Na Mercy Machange, HEET-UDSM***



***Teknolojia Mpya:*** *Baadhi ya vifaa vya kisasa vilivyonunuliwa kupitia Mradi wa HEET kwa ajili ya kusaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kupitia Mradi wa HEET, kimepiga hatua kubwa katika elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum kuanzia ununuzi wa vifaa vipya vya teknolojia ya kisasa hadi mifumo jumuishi ya huduma.

Kwa mujibu wa Dkt. Lulu Mahai, Mkurugenzi wa Huduma za Jamii na Mratibu wa Masuala ya Jinsia wa Mradi wa HEET-UDSM, Chuo kinafanya mageuzi makubwa yanayolenga kufanya elimu ya juu kuwa jumuishi zaidi na inayowezesha wanafunzi wenye ulemavu kuwa sehemu ya wanufaika.

Chuo kimefanikisha kupatikana kwa vifaa 91 kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vifaa hivyo vinajumuisha kompyuta za mezani, televisheni maizi, vifaa vya kurekodia sauti, mashine za kuchukua maandishi kwa mfumo wa breli, kamera, na printa.

"Hapo awali, wanafunzi wetu wengi walitegemea zana za kizamani kama vile mashine ya kuchapa maandiko ya Perkins Braille, ambayo ni kifaa cha mkono kinachofanana na mashine ya kuchapia, lakini sasa wanaweza kutumia vifaa hivi vya kidijitali kuhifadhi kumbukumbu zao, kupata maudhui ya elimu mtandaoni, kubadilisha maandishi kuwa sauti, na hata kuchapa kazi zao za kitaaluma kama wanafunzi wengine," alisema Dkt. Mahai.

Aliongezea: "Hii ni hatua kubwa katika kukuza uhuru wa wanafunzi na kupunguza utegemezi wa msaada wa nje. Kwa sasa, chuo kinahudumia zaidi ya wanafunzi 160 wenye mahitaji maalum na idadi hii inatarajiwa kuongezeka kadri vifaa zaidi vitakavyopatikana."

Mbali na teknolojia, UDSM pia inawekeza katika miundombinu na ukuzaji wa ujuzi. Hatua kubwa iliyopigwa ni ujenzi wa Jengo la Jinsia na watu wenye mahitaji maalum ambalo litakuwa kituo cha pamoja cha huduma kwa watu wenye ulemavu na msaada wa masuala ya kijinsia. Jengo hili litakuwa alama inayoonekana ya dhamira ya chuo katika kukuza elimu jumuishi.

"Programu za mafunzo kwa wafanyakazi na wanafunzi zimeanzishwa. Programu hizi zinajumuisha mafunzo kwa vitendo kwa kutumia teknolojia saidizi, pamoja na warsha kuhusu ukatili wa kijinsia, uongozi, na ujasiriamali," alisema Dkt. Mahai.

Dkt. Mahai aliongeza kuwa walimu na wafanyakazi wasaidizi pia wamepatiwa mafunzo ya kujengewa uwezo ili kuboresha ubora wa huduma zinazotolewa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, huku wanafunzi wakipatiwa stadi za kufanikisha maisha yao katika 'soko la ajira' ili waweze kuajiriwa au kujiajiri.

"Mafanikio yetu makubwa ni kuwapa wanafunzi zana na stadi za kusimamia ujifunzaji wao wenyewe. Kwa sasa maisha ni dijitali na wanafunzi wetu wako tayari kwa hilo," alisisitiza Dkt. Mahai.

### *Teknolojia na mustakabali wa ujifunzaji jumuishi*

Prof. Kwame Ibwe wa Idara ya Uhandisi Elektroniki na Mawasiliano ya Simu, UDSM na Mtaalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa Mradi wa HEET-UDSM, alibainisha nafasi muhimu ya teknolojia katika kufanya mageuzi ya kielimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

"Zana za kisasa zinawawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalumu kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji wa ana kwa ana na mtandaoni. Hivi sasa tuna fursa ya kujumuisha programu saidizi na wakati huohuo majukwaa ya ujifunzaji mtandaoni yanashughulikia mahitaji ya mtu mmoja mmoja, jambo linalojenga mazingira ya kujifunzia yenye kubadilika na jumuishi zaidi," alisema Prof. Ibwe.

Alisisitiza kuwa teknolojia pekee haitoshi. Mafunzo na usimamizi ni muhimu ili kuhakikisha wanafunzi na walimu wanatumia zana hizo kwa ufanisi. "Si suala la kugawa tu vifaa bali kuna umuhimu wa kuwawezesha wanafunzi na walimu kuvitumia kwa namna yenye tija."

Kama mtafiti kiongozi katika teknolojia za mawasiliano zisizotumia waya na mifumo maizi, Prof. Ibwe anaona elimu jumuishi kama sehemu kuu ya mabadiliko ya kidijitali nchini Tanzania. "Tunapowekeza katika elimu jumuishi, pia tunawekeza katika ubunifu na maendeleo ya nchi."

Kupitia Mradi wa HEET, UDSM inakuwa mfano maridhawa wa namna vyuo vikuu vinavyoweza kuongoza katika elimu jumuishi. Kwa kuchanganya teknolojia ya kisasa, miundombinu mahususi na mifumo madhubuti ya ufundishaji, chuo kitaweza kuwasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalum kustawi kitaaluma na kimaisha.

# Viongozi Wasisitizwa Kuwa Kichocheo cha Utafiti na Ubunifu

***Na Wilson Remmy, HEET-UDSM***

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimehitimisha warsha ya mafundo na tafakuri kwa viongozi wake huku viongozi hao wakipokea maelekezo kadhaa kutoka serikalini: Viongozi hao wametakiwa kuwa kichocheo katika utafiti, ubunifu na ubora wa kitaaluma.

Maelekezo hayo yametolewa na Mgeni Rasmi, Profesa Carolyne Nombo, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (MoEST), wakati akifunga rasmi mafundo hayo ya siku tatu.

Mafuno hayo yaliyokuwa na kaulimbiu isemayo "Kukuza Umahiri wa UDSM Kupitia Uongozi wa Kimkakati na Kiubunifu" yaliyowakutanisha pamoja viongozi waandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pamoja na vyuo vyake vishiriki vya DUCE na MUCE yalifanyika tarehe 2 hadi 4 Juni 2025, katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere kilichopo Kibaha.

Prof. Nombo alisisitiza kwamba viongozi wa vyuo vikuu hawapaswi kufanya utawala wa kimazoa bali wanapaswa kuwa kichocheo cha mabadiliko kupitia utafiti wenye tija, ubunifu wenye matokeo na shughuli za kitaaluma zinazozingatia maadili.

"Uongozi wa chuo kikuu lazima uwe injini inayoendesha utafiti bora na matokeo ya tafiti za kitaaluma yanayochangia maendeleo ya kitaifa", alisema.

Aliipongeza menejimenti ya UDSM kwa kujiimarisha kwake katika kuandaa uongozi wenye maono na kuwahimiza viongozi wake kutumia vema mageuzi yanayoendelea ya kitaifa na uwekezaji katika elimu ya juu. Hii ni pamoja na kuimarishwa kwa ufadhili kupitia Mfuko wa Taifa wa Utafiti na Ubunifu (TTIF) na utekelezaji wa Mradi wa HEET, ambapo UDSM na vyuo vyake vishiriki ilipatiwa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 66.

Akizungumza katika hafla hiyo, Makamu Mkuu wa Chuo, Profesa William A. L. Anangisye, aliwashukuru washiriki na kueleza kuridhishwa kwa dhati na ushiriki pamoja na tafakuri kwa washiriki katika kipindi chote cha warsha. Alibainisha kuwa warsha hiyo ilitoa fursa muhimu kwa viongozi kuoanisha majukumu yao na Dira ya Chuo Kikuu.

"Nafasi ya Uongozi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni fursa na wajibu wa kipekee. Tunapaswa kuongoza kwa uadilifu, uwajibikaji, na kujitolea huku tukizingatia ubora katika ufundishaji, utafiti na na majukumu mengine ya kiutumishi," alisema Prof. Anangisye.

Aliwataka viongozi wapya walioteuliwa na wale wanaoendelea kutumia maarifa waliyopata kutoka kwenye warsha hiyo kuimarisha ushirikiano, ubora wa kitaaluma, na uthabiti wa kitaasisi.




***Kuonesha Njia:*** *Katibu Mkuu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo (katikati- waliokaa) akiwa na baadhi ya viongozi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wakiongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye (wa tatu kushoto-waliokaa) mara baada ya Katibu Mkuu kufunga semina ya viongozi wa UDSM iliyofanyika katika Shule ya Uongozi, Kibaha, Pwani, mwezi Juni, 2025.*

### *Kushughulikia Mahitaji ya Kiuongozi Yanayozingatia Mazingira Changamani*

Mwenyeji wa warsha hiyo, Prof. Bernadeta Killian, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo - Mipango, Fedha na Utawala, akitoa mtazamo wa jumla kuhsu warsha hiyo, alieleza kuwa warsha hiyo iliandaliwa kwa lengo la kuwajengea washiriki uwezo wa kushughulikia mahitaji ya kiuongozi yanayozingatia mazingira changamani ya Chuo Kikuu.

"Tumejadili maeneo ya kimkakati ikiwa ni pamoja na masuala ya kitaaluma, mipango ya kifedha, usimamizi wa rasilimaliwatu, usimamizi wa kitaasisi, utawala wa kidijitali, maendeleo ya utafiti, na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kitaifa kama Mradi wa HEET", alisema.

Prof. Killian aliongeza kuwa warsha hiyo "ilikuwa shirikishi, ikihusisha mawasilisho ya wataalamu, majadiliano katika majopo, ubadilishanaji wa uzoefu, ambao uliwawezesha washiriki kutafakari kwa kina majukumu yao na kushirikiana katika vipaumbele vya kimkakati."

Alieleza zaidi: "Hii ilikuwa zaidi ya mafundo, lilikuwa jukwaa la kuthibitisha tena maono yetu ya pamoja na kuimarisha ushikamano wa uongozi katika ngazi zote".

Warsha hii ilishirikisha viongozi waandamizi zaidi ya 200 ikiwa ni pamoja na Manaibu Makamu Mkuu wa Chuo, Marasi wa DUCE na MUCE, Marasi wa Ndaki, Maamidi, Wakurugenzi, Wakuu wa Idara Kuu, Waratibu, Wakuu wa Idara, Wakuu wa Vitengo kutoka kampasi kuu na vyuo vishiriki. Wengi walieleza kwamba warsha imewabadilisha na imekuja kwa wakati hasa ikizingatia mahitaji yanayoongeza kila uchao ya uongozi wa kimkakati katika taasisi za elimu.

Prof. Nombo aliwataka viongozi hao kuyafanyia kazi kwa vitendo mafundo waliyoyapata. "Hakikisheni uongozi wenu unaweka msingi wa ubunifu, utafiti unaozingatia maadili na uboreshaji wa masuala ya kitaaluma. Mnayo mamlaka na sasa mmeongezewa maarifa na kupewa zana zaidi ili kuongoza kwa ufanisi zaidi." alisema Prof. Nombo.

# Ujumbe wa Naibu Mratibu



## Prof. Liberato Haule

**Naibu Mratibu HEET - UDSM**

Kwa niaba ya Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi, ninapenda kutoa shukurani za dhati kwa wadau wetu kwa mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Mradi wa HEET-UDSM. Bila ushirikiano kutoka kwa wadau wetu, bila shaka tusingeliweza kupata mafanikio yaliyopatikana.

Katika kipindi hiki, Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi kilipata misaada mbalimbali kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Timu ya ukaguzi wa ndani ya Wizara ilikagua Mradi ili kuhakikisha taratibu zinazingatiwa kwa kuangazia mahitaji ya serikali na yale ya Mradi. Tunatambua na kuthamini mapendekezo kutoka kwa timu ya ukaguzi, na tunaamini kuwa utekelezaji wake utaboresha zaidi ufanisi katika utekelezaji wa Mradi.

Aidha, Wizara ilitoa msaada kupitia ukaguzi wa mazingira na kijamii na ukaguzi wa maendeleo ya miundombinu. Kupitia mchakato wa ukaguzi na mapendekezo, wataalamu wetu walipata fursa ya kujifunza kutoka kwa wengine na kufanya uboreshaji inapohitajika. Pia, tunathamini ushauri na usaidizi tuliopokea kutoka katika Kitengo cha Kitaifa cha Utekelezaji wa Mradi kupitia mahojiano na mtu mmoja mmoja au mikutano ya waratibu wa Mradi.

Kamati ya Usimamizi wa Mradi pia inathamini ushirikiano ilioupokea kutoka kwa timu ya Benki ya Dunia kwani wakati wowote tulipohitaji msaada timu imekuwa mstari wa mbele kutoa mwongozo na ushauri. Aidha, ushirikiano kutoka kwa wakandarasi mbalimbali, wazabuni vinatambuliwa na kuthaminiwa. Vile vile, timu za KASEMA zimekuwa na mchango mkubwa katika kuisaidia Kamati kushirikiana na wadau katika maeneo mbalimbali ya ujenzi.

Tunatoa shukrani za dhati kwa Menejimenti ya UDSM, Kamati Kuu ya Uendeshaji wa Miradi hapa UDSM, Bodi ya Zabuni ya UDSM, Kamati za Menejimenti, Seneti ya Chuo Kikuu, Kamati za Baraza na Baraza la Chuo kwa ushauri na maelekezo ambayo yanalenga kufanikisha utekelezaji wa Mradi UDSM.

Mradi wa HEET-UDSM umekuwa ukipokea wageni kutoka taasisi mbalimbali zinazotaka kujifunza namna tunavyotekeleza Mradi wetu. Baadhi ya Taasisi tulizozipokea katika kipindi hiki ni Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Tume ya Sayansi na Teknolojia na ujumbe kutoka Sudan Kusini. Wakati wa majadiliano na wadau hao, timu yetu ya PIU nayo pia ilipata uzoefu kutoka kwao ambao pia imetusaidia katika kuboresha hatua mbalimbali za utekelezaji wa Mradi. Tunazikaribisha taasisi nyingi zaidi kuja kujifunza namna ambavyo tumekuwa tukitekeleza Mradi ili nasi pia tujifunze kutoka kwao kupitia ziara hizo.

Tunakutakieni usomaji mwema wa Toleo la Nane
la Jarida la HEET-UDSM



***Utayari:*** *Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET, Prof. Liberato Haule (kulia), mtaalamu wa Ufuatiliaji na Tathmini, Dkt. Egidius Kamanyi (katikati), na Mkuu wa Mawasiliano na Masoko wa UDSM ambaye pia ni mtaalamu wa Mawasiliano ya Umma kwa Mradi wa HEET, Dkt. Dotto Paul Kuhenga (wa tatu kulia), wakiwa kwenye kikao cha waratibu wa Mradi kilichofanyika hivi karibuni mwezi Septemba, 2025 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

# Tahariri

## Matokeo ya Miaka Mitano ya Mradi wa HEET Yameanza Kuonekana

Tukiwa tunaelekea kukamilisha awamu ya mwisho ya Mradi wa HEET katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unaotarajiwa kukamilika mwaka 2026, matokeo yake yameanza kuonekana.

Miaka mitano ya utekelezaji wa Mradi huu sio tu kwamba imefanya maboresho ya kimazingira na kitaaluma, bali pia imeacha alama isiyofutika katika mustakabali wa maisha ya wafanyakazi, wanafunzi na mfumo wa Elimu ya Juu nchini Tanzania.

Ushirikishwaji wa wadau umekuwa msingi wa Mradi tokea hatua za awali. Hivi sasa, faida zake zinaonekana wazi. Wakazi wa maeneo ya Kagera, Lindi, na kutoka Taasisi ya Sayansi za Bahari - Zanzibar (IMS) sio tu kwamba wamepata ajira wakati wa ujenzi lakini pia wamejenga imani ya kuwa sehemu ya watekelezaji wa Mradi katika maeneo yao.

Mbinu hii shirikishi imeimarisha uhusiano, imejenga imani, na kuweka wajibu wa pamoja wa kulinda rasilimali hizi za kitaaluma mara zinapoanza kutumika. Shauku ya wakazi wa maeneo haya ni kuona mafunzo yakianza kutolewa katika kampasi hizi na hivyo kuwa ithibati ya namna ambavyo ushiriki wa wanajamii umekuwa na matokeo ya kujivunia.



***Uongozi:*** *Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo wakiwa na baadhi ya viongozi na watumishi wa UDSM walipotembelea Mradi wa UDSM-HEET mwaka 2024.*

Mradi wa HEET pia umezingatia suala la usalama na uwajibikaji. Uzingativu wa masuala ya kiusalama katika maeneo yote ya miradi ya ujenzi umebadili fikra za wakazi wa maeneo hayo na wafanyakazi kuhusu miradi ya maendeleo inayofanywa na Chuo Kikuu. Ujenzi ulioanza katika hatua za awali ukihusisha vumbi jingi na kelele za ujenzi, hivi sasa umeibua majengo ya mfano yaliyozingatia taratibu na ubora wa kiwango cha juu. Miradi hii pia iliweka Utaratibu thabiti wa Kushughulikia Malalamiko, kwa lengo la kuhakikisha kwamba kunakuwa na utekelezaji endelevu wa Mradi huku jamii ikishuhudia uwajibikaji na nidhamu wakati wa ujenzi.

Mradi wa HEET umeleta mabadiliko makubwa ndani ya Chuo Kikuu. Mipango ya kuwajengea uwezo viongozi na wafanyakazi wa UDSM umewawezesha kujiimarisha na katika utekelezaji wa majukumu yao. Viongozi wapya wamepata mafunzo ambayo yamewapatia mikakati na mitazamo inayoondana na dira ya UDSM na ulimwengu wenye ushindani. Wafanyakazi waliofadhiliwa na Mradi wa HEET kujiendeleza katika masomo ya Shahada za Umahiri na Uzamivu nje ya nchi wanarejea wakiwa na weledi wa hali ya juu utakaowawezesha kujiimarisha katika ufundishaji, utafiti, na ubunifu katika Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Uwekezaji huu wa makusudi kwa watu unaleta athari kwa wanajumuiya na vitengo mbalimbali vya kitaaluma.

Jukumu la msingi la shughuli za kitaaluma za Chuo limeimarishwa kupitia Mradi wa HEET. Mabadiliko makubwa ya mfumo wa majarida ya utafiti wa UDSM yanalenga kuinua viwango vya kitaaluma, kuimarisha mwonekano na kuleta athari kwa jamii. Wakati huo huo, hatua kubwa ya kimaendeleo imefikiwa katika mapitio ya mitaala. Mapitio ya mitaala yatakifanya Chuo kuwa na mitaala inayoendana na vipaumbele vya kitaifa na inayozingatia mafunzo yaliyopatikana kupitia ziara za ulingalishiviwango zilizofanywa katika maeneo mbalimbali ulimwenguni.

# Tahariri...

Mbali na miundombinu ya kufundishia, Mradi wa HEET umesaidia katika kuimarisha ushirikiano baina ya taaluma na tasnia mbalimbali. Programu ya Uambatizi wa wafanyakazi imekuwa daraja muhimu katika kuendeleza ushirikiano baina ya taaluma na mahitaji halisi katika tasnia mbalimbali ambapo ushirikiano huu umekuza ubunifu na kusaidia katika utatuzi wa matatizo yanayoikabili jamii. Hili limejidhihirisha zaidi kupitia Kituo cha Maendeleo na Uhawilishaji wa Teknolojia (TDTC) ambapo uwekezaji katika eneo hili kupitia Mradi wa HEET umekiongozea Chuo uwezo wa kubuni, kufanya majaribio na kuhawilisha maarifa baina ya tasnia mbalimbali na jamii.

Ujumuishaji pia umepewa kipaumbele katika utekelezaji wa Mradi. Ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum hautazamwi tu kama hatua ya mafanikio katika kuimarisha miundombinu kwa watu hawa bali pia unaonesha namna ambavyo UDSM inavyothamini mahitaji ya makundi mbalimbali. Hali hii inaweka msingi wa kuigwa ambapo Taasisi nyingine pia zinaweza kujifunza kupitia uwekezaji huu.

Tunapotafakari juu ya miaka mitano ya utekelezaji wa Mradi wa HEET, ni dhahiri kuwa hakuna shaka kwamba manufaa ya Mradi yanaonekana wazi na tayari matokeo yake yameanza kubadili hali ya maisha ya jamii. Kuanzia ushirikishwaji wa jamii hadi ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na kujifunzia, ujengaji wa uwezo wa kiuongozi, elimujumuishi na uwezeshaji katika kufanya ubunifu. Matokeo ya Mradi wa HEET yamedhihirisha namna ambavyo chuo kikuu kinaweza kubadilisha mustakabali wa taifa.

Ukiwa imesalia mwaka mmoja tu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinajidhihirisha sio tu kama mnufaika wa Mradi, bali kama mfano wa kuigwa. Mradi wa HEET umebainisha kwamba mabadiliko ya kweli hutokea pale ambapo maono, ushirikiano na uwajibikaji vinapounganishwa pamoja.



***Uhakika wa Malazi:*** *Jengo jipya la malazi lililojengwa chini ya Mradi wa HEET katika kampasi ya UDSM Kagera.*


### Uratibu wa Mradi wa HEET-UDSM

**Mratibu wa Mradi**
Prof. Bernadeta Killian

**Naibu Mratibu wa Mradi**
Prof. Liberato V. Haule

### Timu ya Uhariri


**Mhariri Mkuu &**
**Mtaalamu wa Uhusiano kwa Umma na Mawasiliano HEET-UDSM**
Dkt. Dotto Paul Kuhenga

**Wahariri**
Dkt. Lupa Ramadhani (Kiingereza)
Dkt. Mussa Hans (Kiswahili)

**Waandishi:**
Jackson Isdory
Zamda George
Ally Mambele
Renancy Remmy
Donald Boneka
Remmy Wilson
Mercy Machange

**Mpiga Picha:**
Dickens Dominic

**Msanifu**
Michael Mwakatobe

# Matukio katika Picha

***Mustakabali: Kikao cha 10 cha Kamati ya Kitaasisi ya Usimamizi wa Mradi wa HEET kilichofanyika katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, Kibaha, Mkoa wa Pwani, mwezi Aprili, 2025.***











*Mafunzo ya Vitendo: Baadhi ya watumishi wa UDSM wakishiriki katika programu ya uambatishaji watumishi kwenye taasisi mbalimbali mwaka 2025.*


Bi. Heavenlight Munisi akiwa katika kampuni ya Pivotech



Bi. Catherine James akiwa katika kampuni ya Sunflag Tanzania Ltd-Arusha


Bw. Lusajo Mwamakula akiwa TEMESA Kigoma


Bi. Verynice Temu katika vituo vya JKT, mkoani Mara


Bi. Catherine James wa UDSM akiwa katika eneo la Uchakataji wa Upya wa Maji kwenye Mchakato wa Uchangiaji Rangi


Dkt. Godwine Gadiel akipata Uzoefu wa Vitendo katika Teknolojia ya Nyaya za Nyuzinyuzi.


Bi. Verynice Temu katika vituo vya JKT, mkoani Mara


Bi. Catherine James katika kiwanda cha nguo


Dkt. Rachel Sabuni akiwa Songo Songo Gas Plant


*Kikao cha Wajumbe wa Timu ya Utekelezaji wa Mradi wa HEET-UDSM*

# Mikakati ya KASEMA Yaimarisha Uendelevu wa Mradi wa HEET na Ushirikishwaji wa Jamii

*Na Jackson Isdory na Renancy Remmy, HEET-UDSM*



*Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Dkt. Liberato Haule (kushoto), Diwani wa Kata ya Chukweni, na Dkt. Daudi Msangameno (wa pili kulia) akimwakilisha Mkurugenzi wa Taasisi ya Sayansi za Bahari (IMS), wakikabidhi vitendea kazi kwa Katibu wa kamati ya Mfumo wa Kushughulikia Maoni na Malalamiko (GRM) inayojulikana kama KASEMA, wa IMS, Zanzibar.*



*Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Mipango, Fedha na Utawala na Mratibu wa Mradi wa HEET, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. Bernadeta Killian (katikati) na viongozi wa Wilaya ya Lindi, wakikabidhi vitendea kazi kwa Katibu wa kamati ya Mfumo wa Kushughulikia Maoni na Malalamiko (GRM) inayojulikana kama KASEMA, katika eneo la Ngongo, Mkoa wa Lindi.*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimeimarisha uendelevu wa miradi na ushirikishwaji wa jamii kwa ufanisi katika kampasi zake kupitia kamati za Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko ujulikanao kama KASEMA, chini ya Mradi wa HEET.

Katika mazungumzo na jarida hili, viongozi wa UDSM, maafisa na wanajamii kutoka kampasi na maeneo mbalimbali yanayohusika na utekelezaji wa Mradi, walisisitiza kuwa mfumo huu umeongeza uzingatiaji wa taratibu, unaimarisha ushirikiano na jamii, na kuchangia katika uendelevu wa jumla wa Mradi wa HEET chuoni.

"Kama chuo kikuu, tuna jukumu la kimaadili na kitaasisi la kuhakikisha kwamba maendeleo yanakuwa jumuishi, yenye uwazi na endelevu. Mfumo wa KASEMA umedhihirisha dhamira hii kwa kutoa nafasi kwa wadau wote, kuanzia maafisa wa serikali hadi wakazi, kushiriki katika kuboresha mustakabali wa elimu ya juu," alisema Profesa Bernadeta Killian, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo anayeshughulikia Mipango, Fedha na Utawala, na Mratibu wa Mradi wa HEET wa UDSM.

Aliongeza kuwa jukumu la mfumo wa KASEMA katika kukuza imani na uwajibikaji umewasaidia wadau kujihisi salama na kuwa na imani katika usimamizi wa Mradi.

Kwa mujibu wa Dkt. Edmund Mabhuye, Mtaalamu wa Maendeleo ya Mazingira wa UDSM-HEET, mfumo wa KASEMA ni nyenzo muhimu ya Mradi wa HEET ambao umechochea uzingatiaji wa taratibu, kuimarisha ushirikiano na jamii, na kuhakikisha kwamba manufaa ya uwekezaji wa Mradi yanaenea nje ya Chuo Kikuu, yakileta athari chanya kwa jamii inayozunguka maeneo ya Mradi pamoja na wadau wa serikali.

"Ni jukwaa lililoundwa kwa utaratibu na kwa uwazi lililoanzishwa kwa ajili ya kupokea, kushughulikia na kutatua malalamiko na matatizo yanayotokana na upangaji na utekelezaji wa shughuli za Mradi wa HEET. Jukwa hili linahusisha uchunguzi wa kina, mawasiliano ya wazi, na dhamira ya kutoa suluhisho la haki na lisilo na upendeleo," alisema Dkt. Mabhuye.

"Aliongeza kuwa mfumo huo unafanya kazi kama daraja la mawasiliano ya pande mbili kati ya Chuo Kikuu, wakandarasi, watekelezaji wa Mradi, mamlaka za mitaa, jamii zinazozunguka, na wasimamizi wa serikali ili kuhakikisha kuwa changamoto zinashughulikiwa kwa uwazi na kwa usawa"

"Kamati inaundwa na wawakilishi watano wa makundi mbalimbali. Kila kamati huundwa kulingana na muundo na eneo la Mradi, huku ikihakikisha uwakilishi madhubuti wa usawa wa kijinsia, makundi yaliyosahaulika, viongozi wenye ushawishi na viongozi wa jamii," alisema Dkt. Mabhuye.

Akaendelea kufafanua: "Ili kupandikiza utamaduni wa utii wa taratibu na uendelevu, KASEMA imeanzisha hatua mbalimbali ya kimkakati ikiwamo: mafunzo kwa timu za

*Inaendelea Uk. 21...*

...inatoka Uk. 20

Mradi, wakandarasi na viongozi wa jamii kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko; ulinzi wa mazingira na taratibu za kuzingatiwa; kuanzisha mifumo ya ufuatiliaji ili kufuatilia uzingatiaji wa viwango vya afya, usalama na mazingira; vikao vya majadiliano kwa ajili ya kupeana mrejesho na kukuza uwajibikaji wa pamoja; pamoja na kuhamasisha mbinu rafiki kwa mazingira katika ujenzi na maendeleo ya jamii."

Prof. Liberato Haule, Naibu Mratibu wa Mradi wa UDSM-HEET, alieleza kuwa KASEMA ina jukumu kubwa katika kukuza ujenzi wa uwezo, uhakiki wa ubora, na uendelevu.

Alibainisha kuwa mfumo huu unahakikisha utoaji wa taarifa kwa wakati na kwa usahihi; kulinda Mradi; kusaidia katika kuelewa mahitaji ya jamii; kuelekeza manufaa kwa jamii kama vile ajira, mauzo ya vifaa, na usambazaji wa chakula; pamoja na kuwezesha tathmini za mara kwa mara kuhusu ubora na thamani ya fedha.

"Ushirikishwaji wa jamii umefanikisha kuibuliwa kwa mabalozi wengi zaidi wa Mradi. Hivi sasa tuna mifumo inayotegemea takwimu ambayo mbali na kuisaidia UDSM inaiwezesha serikali kupata nyenzo za kufuatilia maendeleo na kutenga rasilimali kwa ufanisi," alisema Prof. Haule.

Alibainisha kuwa kupitia KASEMA, shughuli kadhaa zilizokuwa zimelengwa zimekuwa zikitekelezwa ili kukuza utamaduni thabiti wa zingatiaji wa taratibu, zikiwamo kujengea uwezo, kukuza uelewa, na kukuza dhana ya umiliki.

Vilevile, Prof. Haule alifafanua kwamba Mradi wa HEET ni zaidi ya majengo na vifaa: "Mradi pia unalenga kuanzisha mifumo na taratibu ambazo zitatumika kwa vizazi vya sasa na vijavyo vya wanafunzi na watafiti. Kupitia KASEMA, tunaweka mfumo endelevu katika elimu ya juu."

"Ushiriki wa jamii umekuwa alama kuu ya mafanikio ya Mfumo wa Kushughulilia Malalamiko. Mrejesho wa wadau umeongeza imani katika usimamizi wa Mradi, huku kukiwa na manufaa dhahiri kama vile uzalishaji wa ajira, haki ya matumizi ya ardhi, na kuboresha maisha," aliongeza.

Kiongozi wa jamii na mkulima kutoka Kagera alieleza: "Hapo awali tulikuwa na wasiwasi kuhusu matumizi ya ardhi na upatikanaji wa maji. Sasa, kupitia KASEMA, tunashirikishwa kikamilifu katika kufanya uamuzi, na matatizo yetu yanashughulikiwa haraka."

Vivyo hivyo, katika Kampasi ya Ruangwa mkoani Lindi, mwanajamii mwenye ulemavu wa viungo alionesha matumaini kwa kusema: "Kampasi hii inaleta ajira na fursa kwa vijana wetu. Shughuli za KASEMA zimehakikisha uwazi, na sasa tunauamini mchakato huu kuliko hapo awali."

KASEMA inadhihirisha kuwa maendeleo shirikishi ni endelevu zaidi, hususan katika miradi ya kimkakati kama HEET. UDSM na mamlaka nyingi za serikali zimetambua jambo hili kama mfano wa kuigwa katika miradi mikubwa ya maendeleo ya baadaye. Kwa kuongeza uwazi na kupunguza migogoro, mfumo huu unaunga mkono mikakati ya kitaifa kuhusu elimu ya juu na maendeleo ya miundombinu.

"Mpango huu unaimarisha uhusiano kati ya vyuo vikuu, jamii, na serikali. Unahakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kwa ufanisi na kila raia anaona manufaa halisi," alibainisha Dkt. Lulu Mahai, Mkurugenzi wa Huduma za Kijamii na Mratibu wa Masuala ya Kijinsia wa Mradi wa HEET-UDSM.

Mafanikio ya KASEMA yanaakisi dhamira ya pamoja kati ya UDSM, taasisi za serikali, na jamii za wenyeji. Kwa pamoja, washirika hawa wanabadilisha miundombinu ya elimu ya juu huku wakijenga imani na uhimilivu. Lengo kuu ni kuhakikisha KASEMA inabaki kuwa sehemu ya kudumu ya mfumo wa utawala wa UDSM, na manufaa yake yanaendelea hata baada ya Mradi wa HEET.

"Bila kuwa na jukwaa hili, miradi inaweza kushindwa kutekelezeka hata kabla haijaanza. Dhamira yetu ni kuona KASEMA inakuwa sehemu ya utamaduni wa kitaasisi wa UDSM, mfumo wa kudumu wa uwazi, uwajibikaji na ukuaji wa pamoja," alisema Dkt. Mahai.

Kama taasisi kuu ya elimu ya juu nchini Tanzania, kupitia KASEMA, UDSM inaendelea kuonesha kwamba maendeleo yenye tija yanaweza kupatikana nje ya miundombinu ya kuonekana. Mpango huu hauhusu tu utatuzi wa migogoro bali pia unaweka msingi wa utamaduni wa imani, ujumuishi, na uendelevu.

Kwa kuunganisha utawala, ushirikishwaji wa jamii, na usimamizi wa mazingira, UDSM inahakikisha kwamba uwekezaji wake wa leo utaendelea kuwezesha vizazi vijavyo, na kukiweka chuo katika nafasi ya kuwa mfano bora wa mageuzi ya elimu ya juu barani Afrika.



***Ujumuishwaji na Usalama:*** *Mratibu wa Masuala ya Jinsia wa Mradi wa HEET-UDSM, Dkt. Lulu Mahai (wa pili kulia ameketi) akiwa na washiriki wa mafunzo kuhusu ukatili wa kijinsia kwa watoa huduma katika maeneo mbalimbali ya ujenzi wa Mradi wa HEET-UDSM, yaliyofanyika katika Taasisi ya Sayansi za Bahari, Zanzibar.*

# Uzingativu wa Hatua za Usalama na Ushirikishwaji wa Jamii Vyaimarisha Utekelezaji wa Mradi wa HEET

*Na Ally Mambele, HEET-UDSM*



*Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM, Prof. Liberato Haule, akizungumza na waandishi wa habari walipotembelea eneo la ujenzi wa majengo ya HEET-UDSM, Mkoa wa Lindi mwishoni mwa mwaka 2024*



*Waandishi wa habari pamoja na baadhi ya wajumbe wa Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi wa UDSM walipotembelea eneo la ujenzi wa majengo ya HEET-UDSM, Mkoa wa Lindi mwishoni mwa mwaka 2024*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimeimarisha dhamira yake ya ustawi wa wafanyakazi, ushirikishwaji wa jamii, na uendelevu wa miradi kupitia utekelezaji wa hatua za ulinzi na usalama chini ya Mradi wa HEET.

Hatua hizi, ingawa zinaweza kutazamwa kama ucheleweshaji au uongezaji wa gharama za ziada, zimekuwa muhimu kwa mafanikio ya Mradi, kuimarisha uhusiano na jamii huku zikihakikisha kwamba kunakuwa na utendaji mzuri na wenye ufanisi.

Mtaalamu wa Maendeleo ya Mazingira katika Mradi wa HEET-UDSM, Dkt. Edmund Mabhuye, alisisitiza umuhimu wa mbinu hii. "Ushirikishaji wa jamii umekuwa msingi wa maendeleo ya Mradi huu. Katika maeneo ya Kagera na Lindi, tuliwafikia wananchi kupitia mikutano ya hadhara iliyoitishwa kupitia viongozi wao"

Aliongeza kuwa kwenye mikutano hiyo wananchi walielezwa malengo ya Mradi na faida zake kwa jamii inayozinguka Mradi na taifa kwa ujumla. "Wananchi walikuwa na mwitikio chanya na walitoa kama vile kuomba wapewe fursa za kufanya kazi wakati wa ujenzi. Mbinu hii ilipunguza kwa kiasi kikubwa uwezekano wa kutokea kwa migogoro".

Aliendelea kubainisha kuwa ushirikishwaji wa jamii ulisaidia kufanya muundo wa utekelezaji wa Mradi uwe bora na wenye matokeo chanya.

"Hapo awali, mipango ya usanifu ilipendekeza hosteli za wanachuo wa kiume na wa kike ziwe pamoja, suala hili liliibua wasiwasi wa kitamaduni na kimazoea. Hivyo, tukazingatia maoni ya wananchi kwa kutenganisha bweni la wanaume na wanawake badala ya mpango wa awali. Mabadiliko haya yalikuza hisia ya ushirikishwaji na heshima, na kuongeza kukubalika kwa Mradi ndani ya jamii", alisema.

Dkt. Mabhuye alibainisha manufaa ya uzingativu wa masuala ya usalama katika hatua za ujenzi. "Wanajamii sasa wanatambua kuwa wao ni sehemu ya Mradi, na kuna uwezekano mkubwa wa kutoa taarifa pale ambapo watakuwa na shaka, ikiwa ni pamoja na wizi katika mchakato wa utekelezaji wa Mradi. Suala hili limeimarisha sana usalama katika maeneo ya Mradi".

"Wakati huo huo, kwa kuzingatia kikamilifu itifaki za usalama, tumepunguza majeraha ambayo yangeweza kuwapata wanajamii au watekelezaji wa Mradi mahali pa kazi. Lengo ni kuhakikisha kuwa hakuna mfanyakazi au mwanajamii anayeathirika wakati wa utekelezaji wa Mradi", aliongeza Dkt. Mabhuye.

Wanajamii wameunga mkono maoni haya mazuri. "Hapo awali, tulikuwa na wasiwasi juu ya ajali za magari ya mizigo yanayopita hapa kijijini kwetu, lakini sheria za usalama zimepunguza hatari hizo. Sasa tunajisikia salama zaidi kutembea na watoto wetu", amesema Mariam Juma, mkazi wa karibu na eneo la Mradi wa Lindi.

Vilevile, Petro Agapitius, mkulima kutoka Kagera, alipongeza juhudi za ushirikishwaji wa jamii. "Viongozi wa Mradi walitusikiliza na kuheshimu utamaduni wetu wakati wa kupanga ujenzi wa hosteli za wanafunzi. Hii ilionyesha ni kwa namna gani wanajali utamaduni wetu. Inatufanya tujivunie kuunga mkono Mradi na kuulinda kama wetu". alisema Petro.

Kwa mtazamo wa kitaasisi, UDSM inachukulia matokeo haya kama ithibati kwamba ushirikiswaji wa jamii katika hatua mbalimbali za Mradi una manufaa makubwa katika kufanya mageuzi ya kijamii. Chuo Kukuu cha Dar es Salaam kinaamini kwamba kuwashirikisha wanajamii katika hatua za usanifu na utekelezaji wa Mradi kunachangia katika kuhakikisha kuwa kunakuwa na uendelevu na ukubalifu wa muda mrefu wa Mradi.

Akitoa mtazamo wa jumla kuhusiana na suala hili, Dkt. Mabhuye alisisitiza kuwa "Utaratibu uliotumiwa na UDSM unadhihirisha kwamba uendelezaji wa miundombinu unapozingatia ushirikwaji wa wanajamii na masuala ya usalama unaweza kuleta mageuzi makubwa katika jamii. Tunachokiona hapa ni mfano wa namna miradi kama hii inavyotekelezwa maeneo mengine".

# Ujumbe kutoka Sudani Kusini Wapongeza Maendeleo ya Mradi wa HEET UDSM

*Na Jackson Isdory, UDSM-HEET*



***Ulinganishi Viwango:*** *Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Utafiti, Prof. Nelson Boniface (katikati, mstari wa mbele) akiwa na baadhi ya wajumbe wa Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi wa HEET-UDSM na ujumbe kutoka Wizara ya Elimu ya Jumla na Taasisi (MoGEI) ya Sudan Kusini, ukiongozwa na Mhe. Kachuol Mabil Piok, mwezi Julai, 2025. Ujumbe huo uliItembelea UDSM kwa lengo la kujifunza utekelezaji wa Mradi wa HEET.*

Katika harakati za kujenga ushirikiano wa kikanda na kubadilishana uzoefu katika maendeleo ya elimu, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kilipokea ujumbe wa viongozi waandamizi kutoka Wizara ya Elimu ya Jumla na Mafunzo kutoka Sudani Kusini (MoGEI).

Ziara hiyo, iliyofanyika Alhamisi, tarehe 17 Julai 2025, ililenga katika kufanya ulinganishi viwango kwa Mradi wa HEET unaofadhiliwa na Benki ya Dunia na ilidhihirisha ushirikiano wa dhati kati ya mataifa haya mawili, ikiangazia wajibu wa Taasisi za elimu katika kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Ziara hiyo ililenga kujifunza masuala mbalimbali kutokana na utekelezaji wa Mradi wa HEET nchini Tanzania, ikiwa ni pamoja na utawala wa kimkakati na uongozi wa kitaasisi, na hivyo kusaidia katika jitihada zake za kujenga ujuzi kwa maendeleo ya watu wa Sudani Kusini.

"Ushirikiano huu unadhihirisha jukumu la UDSM katika kufanikisha ipasavyo matarajio ya Afrika. Ushirikiano wetu na Sudani Kusini unajikita katika mtazamo wetu wa pamoja katika masuala ya umajumui wa Afrika, mfumo wa elimu, na ushirikiano endelevu," alisema Prof. Nelson Boniface, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo - Utafiti kutoka UDSM.

Prof. Boniface alisisitiza kwamba, mbali na kutekeleza Mradi wa HEET kwa ufanisi, UDSM imedhamiria kuwa kinara kikanda katika utoaji wa elimu ya juu, mafunzo ya ualimu, na uandaaji wa sera. Alitolea mfano ushirikiano unaoendelea baina ya UDSM na Chuo Kikuu cha Juba katika ufundishaji wa lugha ya Kiswahili, uandaaji wa mitaala na utafiti.

Mhe. Kachuol Mabil Piok, Msaidizi wa katibu mkuu kutoka Wizara ya Elimu ya Jumla na Mafunzo, Sudani Kusini, alielezea kuwa ziara hiyo imefanyika wakati mwafaka na imekuwa na manufaa ya hali ya juu.

"Tumevutiwa sana na uongozi wa sekta ya elimu nchini Tanzania pamoja na uwajibikaji wa kitaasisi. Mafunzo tuliyoyapata kupitia Mradi wa HEET ni muhimu sana na yatatusaidia katika Mpango wa Elimu ya Sekondari na uboreshaji wa mifumo ya maendeleo ya walimu", alisema.

Ziara hiyo ilionyesha dhamira ya dhati ya kimkakati ya serikali zote mbili chini ya uongozi wa Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan wa Tanzania na Mhe. Rais Salva Kiir Mayardit wa Sudani Kusini katika kuboresha elimu kama msingi wa maendeleo ya kitaifa, uwezeshaji wa vijana, na maendeleo ya watu.

Ujumbe wa Sudani Kusini uliongozwa na Mhe. Piok na Mhe. Balozi. Gloria John Mambai (kaimu Balozi, Ubalozi wa Sudani Kusini nchini Tanzania), pamoja na maafisa waandamizi Thadeo Kuntembwe (Mratibu wa Mradi wa BSHCDSS), Victor Dut Chol, Samuel Dem Marier, John Lujang Wani, Majuch Madul Abor, Elizabeth Yom, Daniella Achol, na Kual Amath (Katibu wa Kwanza).

Kwa upande wa UDSM, wageni hawa walipokelewa na Prof. Boniface Naibu Makamu Mkuu wa Chuo- Utafiti na Prof. Liberato Haule (Naibu Mratibu wa Mradi wa HEET). Wengine waliokuwapo ni Dkt. Lulu Mahai, (Mratibu wa Masuala ya Jinsia/ Watu wenye Mahitaji Maalum wa HEET-UDSM), Dkt. Fatuma Simba (TEHAMA/Ushikiano na Tasina), Dkt. Augustina Alexander (Umataifishaji), na Prof. George Kahangwa (Shule Kuu ya Elimu).

*Inaendelea Uk. 24...*

...inatoka Uk. 23

Mijadala baina ya wageni na wenyeji ilijikita katika maeneo sita ambayo ni, mifumo ya uendeshaji kwa ajili ya programu za ujifunzaji kwa mwendokasi na njia za uidhinishaji wa walimu; ubunifu katika ufundishaji, uthibiti ubora, na kuwajengea uwezo walimu; mapitio ya mtaala inayoendana na mahitaji ya soko la ajira na njia ya ushirikishwaji wa jamii; sera za elimu zisizo rasmi kwa maeneo yaliyokubwa na migogoro.

Maeneo mengine ni mabadiliko ya kidijitali kupitia Mifumo ya Usimamizi wa Mafunzo, na Kampasi maizi; na mipango ya pamoja ya utafiti na ubadilishanaji maarifa ili kuendeleza mageuzi yanayotokana na ushauri wa kitaalamu.

### *Mafunzo ya Pamoja kwa Maendeleo ya Kikanda*

Maafisa kutoka Sudani Kusini walionyesha nia ya kipekee katika kujifunza kutoka UDSM kuhusu matumizi ya shule za sekondari kama vituo vya kufanyia mazoezi ya kujifunzia na sera zake zinazounga mkono mifumo ya elimu isiyo rasmi pamoja na namna ya kushughulikia tofauti za kielimu katika maeneo yaliyokuwa na migogoro.

Aidha, walijifunza kuhusu Mfumo wa Ujifunzaji kwa Njia ya Mtandao (LMS) wa UDSM, Mafunzo mbalimbali yanayotolewa kwa njia ya mtandao na jitihada za kuwa na Kampasi maizi ikiwa ni hatua ya mageuzi ya kidijitali. Lengo la ulinganishiviwango ni kuona namna ambayo mifumo hii inavyoweza kutumika katika vyuo vya mafunzo ya walimu nchini Sudani Kusini

"Ziara hii inaimarisha nafasi ya UDSM sio tu katika utekelezaji wa Mradi wa HEET, bali Chuo kinaendelea kuwa kinara kikanda katika mabadiliko ya elimu. Inaonesha nafasi muhimu ya vyuo vikuu katika uimarishaji wa sekta ya umma kikanda," alisema Prof. Haule.

Ziara hii muhimu ya ulinganishiviwango inathibitisha ukuaji wa ushawishi wa UDSM katika eneo hili kama kinara wa fikra katika mabadiliko ya elimu. Zaidi ya eneo la utekelezaji wa Mradi, UDSM inaweka msingi wa mageuzi makubwa ya elimu yenye mafanikio, jumuishi katika nchi za Afrika Mashariki.

Ushirikiano unaoendelea katika mfumo wa elimu baina ya Tanzania na Sudani Kusini ni ishara ya nguvu ya diplomasia ya maarifa, unaoweka msingi mpya ya ushirikiano wa kikanda, ustahimilivu, na ustawi wa pamoja.





***Ushirikiano:*** *Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Utafiti, Prof. Nelson Boniface (wa pili-kushoto, mstari wa mbele, picha ya kushoto) akiwa na baadhi ya wajumbe wa Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi wa HEET- UDSM na ujumbe kutoka Wizara ya Elimu ya Jumla na Taasisi (MoGEI) ya Sudan Kusini, ukiongozwa na Mhe. Kachuol Mabil Piok, mwezi Julai, 2025. Ujumbe huo ulitembelea UDSM kwa ajili ya kujifunza utekelezaji wa Mradi wa HEET.*

## Mfumo wa Ushughulikiaji Malalamiko Wafanikisha Uzingatiaji Madhubuti wa Taratibu katika Utekelezaji wa Mradi wa HEET

(inatoka Uk. 10)

kupitia mbinu endelevu; na kuimarika kwa uhusiano kati ya UDSM na jamii za wenyeji – jambo linalochochea ukuaji wa pamoja na mshikamano wa kijamii; na kuimarishwa kwa uzingatiaji unaopunguza gharama za usimamizi wa serikali na vihatarishi vya uendeshaji na hivyo kuiweka UDSM katika nafasi ya kuwa taasisi ya mfano katika mageuzi ya elimu ya juu barani Afrika.

Dkt. Mabhuye aliongeza kuwa Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko unahakikisha kila eneo linazinagtia viwango vya mazingira, kijamii na kiutawala. "Hii inamaanisha kwamba miundombinu yetu haijengwi ili tu idumu, bali pia ishughulikie mahitaji ya jamii za wenyeji na kuzingatia malengo ya maendeleo ya Taifa".



*Mafunzo kwa wafanyakazi wa utawala na wafanyakazi wapya walioajiriwa hivi karibuni kuhusu muhimu wa kukuza mazingira yasiyo na ukatili wa kijinsia (GBV), yaliyofanyika hivi karibuni katika Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani hivi karibuni.*

# Ushirikishwaji wa Wadau Waonesha Mafanikio katika Mradi wa HEET UDSM

*Na Renancy Remmy, HEET-UDSM*



***Ndoto yatimia:** Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (wa pili kushoto) akitazama ramani inayoonyesha eneo ilipo Kampasi ya UDSM Lindi. Pembeni yake ni Mratibu wa Mradi wa HEET UDSM ambaye pia ni Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Mipango, Fedha na Utawala, Prof. Bernadeta Killian (wa tano kushoto), pamoja na wataalamu wa UDSM na maafisa wa Mkoa waindi.*

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) kimeangazia jukumu muhimu la ushirikishwaji wa wadau katika kufanikisha utekelezaji wa Mradi wa HEET ambao umekuwa na wenye manufaa yanayoonekana dhahiri katika kampasi zake nchini Tanzania.

Kwa mujibu wa Dkt. Edmund Mabhuye, Mtaalamu wa Mazingira kwenye Mradi wa HEET, kuwahusisha wadau kuanzia hatua za awali za Mradi huo kumeimarisha kwa kiasi kikubwa maendeleo na ushiriki wa jamii.

Dkt. Mabhuye alieleza kuwa mpango huo sio tu kwamba umeimarisha uhusiano kati ya Chuo Kikuu na jamii zinazozunguka maeneo ya miradi bali pia unahakikisha kuwa maendeleo yanaendelea kuwa jumuishi na endelevu.

"Katika Kampasi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere-Mlimani, ambapo ujenzi mkubwa unaendelea, ushirikishwaji wa wadau umetoa fursa kwa wakazi wa eneo hilo kupata ajira huku kukiwa na uwajibikaji wa pamoja katika kulinda na kusaidia kuendeleza miundombinu", amesema Dkt. Mabhuye.

Ameongeza kuwa mbinu za aina hiyo zimezingatiwa pia katika kampasi mpya zinazoendelea kujengwa katika mikoa ya Kagera na Lindi, na katika Taasisi ya Sayansi za Bahari -Zanzibar.

"Kupitia ushirikishwaji wa wadau, wakazi wa eneo la Mradi hawajisikii kutengwa; wanashiriki, wanapata ajira, na wanakuza dhana ya umiliki wa miradi hii. Uhusiano huu pia unawafanya wakandarasi na watekelezaji wengine wa Mradi kufanya kazi kwa kuwajibika zaidi huku wakizingatia zaidi viwango vya usalama na uhusiano wa kijamii unaozingatia usawa," ameeleza Dkt. Mabhuye.

Mbali na fursa za ajira, ushiriki wa wadau umejenga daraja la uaminifu na ushirikiano. Wakandarasi na watekelezaji wa Mradi wanahimizwa kushirikisha jamii mara kwa mara wanaposhughulika na maswala ya kiusalama, kimazingira, na changamoto kilijistiki.

"Mtazamo huu wa ushirikishaji wa jamii umepunguza migogoro na kuifanya miradi kuendelea vizuri ikilinganishwa na mitindo ya kijadi iliyokuwa imezoeleka," Ameongezea Dkt. Mabhuye.

Alisisitiza kuwa mikakati hiyo shirikishi imekiwezesha Chuo kutekeleza Mradi wa HEET kwa ufanisi zaidi, kupunguza msuguano na ucheleweshaji unaohusishwa na maendeleo makubwa ya ujenzi. Mbinu hiyo pia imepaisha sifa za taasisi, na kujenga imani ambayo itakisaidia Chuo katika mipango yake ya baadaye.

"Ushirikishwaji huu unaweka msingi madhubuti unaoweza kuigwa na taasisi nyingine. Hali hii inadhihirisha kwamba viwango vinapozingatiwa na jamii kuthaminiwa, miradi sio tu inafikia malengo yake bali pia inaacha alama ya kuigwa na kuweka misingi imara ya ushirikiano kwa siku zijazo," Amesisitiza Dkt. Mabhuye.

*Inaendelea Uk. 27...*

# Ushirikishwaji wa Wadau Waonesha Mafanikio katika Mradi wa HEET UDSM

*(Inatoka Uk. 25)*

***Kaya Nyingi Zanufaika***

Wakazi wanaozunguka eneo la Mradi pia wamethibitisha faida wanazozipata kwa njia hii ya ushirikishwaji. Mkazi mmoja anayeishi karibu na eneo la ujenzi katika kampasi ya Lindi, alieleza kuwa Mradi huo umeleta unafuu kwa kaya nyingi.

"Watu wanapata kazi hapa, hata ikiwa ni ya muda. Pia tunafurahi kwa sababu siyo tu kwamba tunashuhudia chuo hiki kujengwa kwenye ardhi yetu bali pia namna tunavyoshirikishwa katika hatua za ujenzi. Tutahakikisha tunakilinda kwa sababu kimekuwa ni sehemu ya jamii yetu", alisema mkazi huyo.

Mfanyabiashara mmoja ambaye yuko karibu na eneo la ujenzi katika kampasi ya Kagera alibainisha faida zisizo za moja kwa moja za kiuchumi. "Biashara imeimarika tangu wafanyakazi wafike. Tunauza vyakula, vifaa vya ujenzi na vitu vingine vidogovidogo. Muhimu zaidi, ni kwamba tunajisikia kuheshimiwa kwa sababu Chuo kinatusikiliza na kuhakikisha usalama wetu unazingatiwa wakati ujenzi ukiendelea".

Wakati Mradi wa HEET ukiendelea kubadilisha mazingira ya elimu ya juu nchini Tanzania, mkabala shirikishi unaozingatiwa na UDSM unarejelewa kama njia bora ya kuwianisha maendeleo ya kitaaluma na mageuzi ya kijamii na kiuchumi. Uwezo wa chuo kuunganisha masuala ya kitaaluma na matarajio ya jamii unabainisha njia bora na endelevu ya maendeleo ya elimu nchini.



***Ushirikishwaji wa Wadau:*** *Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, akizungumza na wakazi wa Mkoa wa Lindi kuhusu kampasi hiyo mpya ya UDSM katika mkoa wao, mwezi Agosti, 2023.*

# Programu ya Uambatishaji Wafanyakazi wa UDSM Kwenye Tasnia Yabadilisha Mtazamo wa Kitaaluma

*(inatoka Uk. 9)*

(CoICT) alipata stadi muhimu katika kutumia teknolojia ya nyaya za mawasiliano yanayosafrishwa kwa mwanga (fibre optics), akitumia Optical Time Domain Reflectometer (OTDR) kupima maeneo ya kuunganisha na ubora wa mawimbi, jambo ambalo ni muhimu kwa sekta ya miundombinu ya kidijitali.

Katika sekta ya ufugaji viumbe maji, Bi. Verynice Temu kutoka Shule Kuu ya Sayansi Akua na Teknolojia ya Uvuvi (SoAF) alipata mafunzo katika kambi za JKT mkoani Mara, akijihusisha na kutenga vifaranga, uzalishaji wa chakula cha samaki na kilimo cha Azolla kama mbadala endelevu wa chakula.

Programu hii imewapa wanataaluma fursa ya kipekee ya kukabiliana moja kwa moja na changamoto mahusussi za kila sekta, na kupata uelewa wa thamani utakaoboresha kwa kiasi kikubwa ufundishaji na utafiti wao wawapo UDSM.

Kupitia Mradi wa HEET, UDSM inafanya uwekezaji wa kimkakati kwa wanataaluma wake kwa kukuza ushirikiano wa muda mrefu na viongozi wa tasnia mbalimbali. Ushirikiano huu hauimarishi tu uwezo wa wafanyakazi bali pia unahakikisha kuwa kizazi kipya cha wahitimu kinaingia katika soko la ajira kikiwa na ujuzi wa vitendo unaolingana na mahitaji ya uchumi wa Tanzania unaokua kila uchao.



***Nadharia na Vitendo:*** *Dkt. Rachel Sabuni (kulia-mstari wa mbele), Mhadhiri katika Taasisi ya Sayansi za Bahari ya UDSM, akiwa katika kiwanda cha kuzalisha gesi cha Songo Songo, Tanzania, kama sehemu ya kundi la pili la programu ya uambatishaji wa watumishi wa UDSM, mwezi Aprili, 2025.*

Ufanisi mkubwa wa awamu ya pili tayari umefungua njia ya ushirikiano mpana zaidi, ikiwamo uandaaji wa mitaala ya pamoja, ongezeko la mafunzo kwa vitendo ya wanafunzi, na programu zaidi za mafunzo ya pamoja.

Programu ya Uambatishaji Wafanyakazi wa UDSM inadhihirisha kuwa mbali na kuwa programu ya ukuzaji taaluma ni mfano wa mabadiliko unaowawezesha walimu, kuboresha ufundishaji wa wanafunzi, na kuchangia moja kwa moja katika maendeleo ya viwanda na uchumi wa Tanzania.

# HEET Yaizatiti UDSM Kufundisha Programu 98 kwa Njia ya Mtandao na Njia Mseto

*Na Renancy Remmy, HEET - UDSM*

Katika mkakati wake wa kuleta mabadiliko ya kidijitali, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), kupitia Mradi wa HEET, kimezindua Mafunzo ya Kujenga Uwezo kwa programu zitazoendeshwa kwa njia ya mtandao na njia Mseto.

Programu hii muhimu, inayotekelezwa chini ya Mradi wa HEET kama sehemu ya utekelezaji wa dira ya UDSM ya kuwa 'Kampasi Maizi,' ilizinduliwa rasmi tarehe 6 Oktoba 2025 katika Ukumbi wa Maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Hafla hiyo ilihudhuriwa na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. William A. L. Anangisye, pamoja na viongozi wengine waandamizi wa chuo, wanataaluma, na wataalamu wa TEHAMA.

Prof. Anangisye aliielezea programu hiyo kama sehemu ya uwekezaji wa kimkakati katika mustakabali wa kuimarisha mfumo wa kidijitali katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Hii ni zaidi ya uzinduzi wa programu ya mafunzo; ni ishara ya uzinduzi wa jambo muhimu katika kutekeleza dira ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambayo inajidhihirisha katika uwekezaji katika mifumo ya dijitali na ukuaji katika masuala ya kitaaluma, unaoendana na mahitaji ya sasa ya kitaifa," alisema.

Aliongeza kuwa, "Kupitia programu hii, tunawatayarisha wanataaluma wetu na wataalamu wa TEHAMA kuwa wawezeshaji katika mwelekeo huu mpya ya elimu, ambao unaweka msisitizo katika masuala ya ubunifu, ushirikishwaji, na ufundishaji kwa njia ya kidijitali."

Prof Anangisye alisisitiza zaidi kuwa programu hii inakiwezesha Chuo kutekeleza kwa ufanisi unaotakiwa mahitaji ya elimu kitaifa na kimataifa. Inasisitiza lengo pana la Chuo kuwa kituo mahiri cha elimu kwa njia ya dijitali, ubunifu, na utafiti ndani na nje ya Tanzania.

Pia aliwataka wanataaluma kutumia mbinu bunifu katika ufundishaji huku wakizingatia utoaji wa elimu yenye ubora wa viwango vya juu, uadilifu, na ushirikishwaji katika utoaji wa elimu kwa njia ya dijitali.

"Wataalamu wa TEHAMA wanatakiwa kuhakikisha uendelevu wa uendeshaji wa mifumo mipya ili kuwezesha utekelezaji wa mabadiliko haya. "Kwa wanafunzi wetu, mifumo hii ni shirikishi, inayozingatia mabadiliko kulingana na mahitaji na inayowezesha kujifunza na kupata uzoefu kwa mawanda mapana zaidi huku ikipanua wigo wa kuimarisha ujuzi wa kujfunza kwa vitendo zaidi," alisisitiza Prof. Anangisye.

### Utoaji wa Elimu Bora katika Zama za Dijitali

Mratibu wa Kituo cha Ujifunzaji kitalifa Dkt. Fatuma Simba alieleza kuwa mafunzo hayo yameandaliwa ili kuwapa watumishi maarifa, ujuzi na ujasiri wa kutoa elimu bora katika mfumo wa kidijitali. Programu hii inaenda sambamba na utekelezaji wa programu 98 za kitaaluma zilizoandaliwa ili kuendeshwa kwa njia ya mtandao na njia mseto ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Dira ya 2061 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

"Kati ya programu 98, programu mbili za shahada ya uzamili zitafundishwa mtandaoni moja kwa moja, wakati programu zilizobaki za shahada ya awali na uzamili zitafundishwa kwa njia mseto," alisema Dkt. Simba.

Dkt. Simba alitaja programu zitakazoendeshwa kwa njia ya mtandao moja kwa moja kuwa ni Digrii ya Umahiri wa Sayansi katika Mpango na Uhandisi wa Usafiri na Stashahada ya Uzamili katika Usimamizi wa Uhandisi. Zote zinatolewa katika Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (CoET).

Aliongeza kuwa: "Mafunzo haya yanawapa wanataaluma wetu na wataalamu wa TEHAMA stadi na maarifa ya kuwawezesha kufanikisha ujifunzaji kwa njia ya mtandao na njia mseto, kuhakikisha kwamba wanafunzi wanafurahia elimu shirikishi, jumuishi na inayozingatia mabadiliko.



***Msingi Imara:*** *Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Prof. William A. L. Anangisye (kulia-mstari wa mbele), akiongoza viongozi na watumishi wengine wa UDSM katika uzinduzi wa Mafunzo ya Kujenga Uwezo juu ya Ufundishaji kwa Njia ya Mtandao na kwa Njia Mseto yanayodhaminiwa na Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET), katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), tarehe 6 Oktoba, 2025.*

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo - Taaluma, Prof Bonaventure Rutinwa, alisisitiza kwamba mafunzo hayo ni zaidi ya mabadiliko katika ufundishaji. "Haya sio tu mabadiliko katika mbinu za ufundishaji bali ni mabadiliko katika mfumo kamili wa namna tunavyoimarisha ubora wa elimu katika zama za dijitali. Ninawahimiza wafanyakazi wetu kushiriki kikamilifu na kuhakikisha kwamba tunazingatia matumizi ya dijitali katika ufundishaji wetu".

Alitaja malengo makuu matatu ya mafunzo hayo kuwa ni uimarishaji wa uwezo, uthibiti wa ubora, na uendelevu kwa njia ya ubunifu. Alisisitiza kwamba washiriki watapata umahiri katika stadi walizonazo na kujiamini katika kutumia teknolojia za kidijitali katika ufundishaji na ujifunzaji.

### Uwekezaji katika Miundombinu ya Kidijitali

Akitoa maelezo kuhusu miundombinu itakayosaidia mabadiliko haya, Naibu Makamu Mkuu wa Chuo- Mipango, Fedha na Utawala na Mratibu wa Mradi wa HEET-UDSM, Prof Bernadeta Killian, alieleza namna ambavyo Chuo kimefanya uwekezaji mkubwa kupitia Mradi huu.

"Kupitia Mradi wa HEET, tumetenga rasilimalifedha ili kufanikisha ujenzi wa miundombinu ya dijitali, kuimarisha ufunzaji na ujifunzaji kwa kutumia teknolojia ya kisasa, na kuboresha ufanisi wa kiutendaji kwa ujumla. Mipango hii inaenda sambamba na mpango wa miaka 10 wa UDSM 2022-2032 wa kuwa na Kampasi Maizi" Alisema Prof. Killian

Prof. Killian aliongeza kuwa majukwaa ya kufundishia na kujifunzia kama vile Moodle LMS, Massive Open Online Courses (MOOC), na Open Educational Resources (OER) yameboreshwa hadi matoleo kwa kuzingatia matoleo ya karibuni, na hivyo kuimarisha upatikanaji wa zana za kidijitali za kujifunzia na kuwa na maudhui shirikishi.

Naibu Makamu Mkuu wa Chuo-Utafiti, Prof Nelson Boniface, kwa upande wake aliangazia dhima ya mabadiliko ya kidijitali katika kuendeleza utafiti na ubunifu. "Zana za kidijitali ni muhimu katika kufanikisha upatikanaji, ubora, na athari chanya za matokeo ya utafiti," Alibainisha Prof. Nelson.

Mafunzo hayo yanaashiria hatua nyingine madhubuti katika safari ya kidijitali ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ikiwawezesha Wanajumuiya wake kufundisha, kujifunza, na kuwa wabunifu kwa kuzingatia mahitaji yanayoendelea ya karne ya 21.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

HEET
HIGHER EDUCATION FOR ECONOMIC TRANSFORMATION

## Mawasiliano


Naibu Mratibu: +255 765 939 958

Mhariri Mkuu: +255 755 172 570

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam,
Jengo la Cranford Pratt,
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere, Mlimani
Barabara ya Chuo Kikuu, 16103 Ubungo
S.L.P. 35091
Dar es Salaam, Tanzania

heet@udsm.ac.tz Heet Udsm www.udsm.ac.tz